# Nipashe

Jumamosi Desemba 21, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580107

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

UNDER THE SAME SUN ARIGATOU INTERNATIONAL GNRC CEFA

215544702




## Watu wasiojulikana wadaiwa kumteka ofisa wa LHRC Dar

UKURASA 3

# Mbowe aanika sababu za Mnyika kumrithi Mashinji

UK. 2




John Mnyika



Vincent Mashinji



Freeman Mbowe





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store


## Wacharuka viongozi wa mtaa kuuza eneo la wazi

UKURASA 2

## Amuua mkewe kisha kujiua

UKURASA 12

**MICHEZO** NIYONZIMA AWATULIZA MASHABIKI YANGA UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mbowe aanika sababu za Mnyika kumrithi Mashinji

Na Enock Charles

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, ametaja sababu za kufanya mabadiliko katika sekretarieti ya chama hicho yaliyohusisha uteuzi wa Katibu Mkuu mpya John Mnyika.

Mbowe (58), amefanya mabadiliko hayo ikiwa ni saa chache tangu afanikiwe kurejea katika kiti chake hicho baada ya kupata asilimia 93 ya kura za wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika jijini Dar es Salaam Jumatano.

Mnyika, ambaye pia ni Mbunge wa Kibamba, amechukua nafasi ya aliyekuwa Katibu Mkuu, Dk. Vicent Mashinji.

Baraza Kuu la Chadema pia limeridhia uteuzi wa Salum Mwalim kuendelea na nafasi yake ya Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na kuteuliwa kwa Mkurugenzi wa Oparesheni na Mafunzo, Benson Kigaila kuwa Naibu Katibu Mkuu Tanzania Bara na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu.

Akizungumza na wajumbe wa baraza hilo jijini jana, Mbowe alisema viongozi wote aliowateua ni watu wanaoaminika na waliokulia na kukomaa ndani ya chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Mbowe alisema safari ya siasa ni ya mafunzo na hivyo alioamua kuwateua ni watu ambao hawatiliwi shaka ndani ya chama hicho.

"Nilioamua kuwateua safari hii ni watu ambao tunawaamini pasipo shaka, wamekulia na kukomaa ndani ya chama chetu," alisema.

**KUTOLIPWA MSHAHARA**

Akizungumza baada ya uteuzi huo, Mnyika alisema jukumu alilopewa ni zito na lisilokuwa na malipo kutokana na utaratibu uliopo ndani ya chama hicho kwa mtu anayeshika nafasi ya uongozi katika chama huku akiwa na nafasi ya kiserikali (ubunge na udiwani) kutokulipwa mshahara na chama.

Mnyika alibainisha kuwa amekitumikia chama hicho kwa nafasi mbalimbali kwa miaka 15 tangu alipojiunga nacho mwaka 2004 akiwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), akianzia kuongoza vijana wa chama hicho kama mkurugenzi wa vijana kabla ya nafasi hiyo kubadilishwa jina na kuwa Baraza la Vijana.

Alisema kuwa akiwa mwanafunzi wa UDSM, alialikwa katika kongamano la vijana lililoandaliwa na Chadema miaka hiyo na moja ya wazo alilolitoa katika kongamano hilo ni kuishauri Chadema kuanzisha mabaraza ya chama, wazo lilomshawishi Mbowe (wakati Mbowe alikuwa ni mwanachama wa kawaida Mzee Edwin Mtei akiwa Mwenyekiti).

Mnyika ambaye aliteuliwa katika nafasi ya Naibu Katibu Mkuu Bara mwaka 2004,

INAENDELEA UK. 8



Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa kampuni ya Sigara (TCC), Godson Killiza (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh.milioni 20 kwa Mbunge wa Temeke, Abdallah Mtolea, kwa niaba ya Umoja wa Wanawake wenye Ulemavu wa viungo Temeke (Uwaviute) katika sherehe zilizofanyika jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mbunge wa Viti Maalum, Mariamu Kisanji (wa tatu kulia). **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Wacharuka viongozi wa mtaa kuuza eneo la wazi

Na Mwandishi Wetu

WAKAZI wa Mtaa wa Ali Hassan Mwinyi, Mikocheni A jijini Dar es Salaam, wameujia juu uongozi wa eneo hilo wakilalama eneo la wazi kuuzwa kwa mwekezaji.

Wamedai tayari mwekezaji huyo waliyemtaja kwa jina moja la Nakiete, ameweka uzio kuzungushia eneo hilo akidai alilipata kwa njia za kisheria. Wananchi hao jana waliandamana hadi kwenye ofisi ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa lakini hawakumkuta kiongozi mkuu wa ofisi hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Salma Zuberi, alidai hajui chochote kuhusu suala hilo na hakuna malalamiko yoyote yaliyofikishwa kwao.

Hata hivyo, kauli hiyo ilipingwa vikali na wakazi wa eneo hilo waliodai suala hilo limekuwapo kwa muda mrefu.

Mjumbe wa eneo hilo, Amani Mero, alieleza kusitikishwa na uamuzi wa kuuza eneo hilo la wazi, akiwashtumu viongozi wenzake wa serikali ya mtaa kufanya uamuzi huo bila ridhaa ya wananchi.

"Watoto wetu hawana sehemu ya kuchezea na eneo hili lilikuwa na miti mingi lakini tangu apewe mwekezaji, miti yote imekatwa na eneo la kuwekewa uzio kwa siku moja chini ya ulinzi mkali," alidai.

Richard Riwa, mkazi wa eneo hilo, alidai mgogoro kati ya mwekezaji na wakazi wa mtaa huo ulianza baada ya wananchi kubaini eneo hilo limeuzwa ilhali kwa miaka mingi limekuwa likitumiwa kama eneo la wazi lililosajiliwa kwa Na. 628.

"Mwaka jana, tuligundua kwamba (mwekezaji) alikuwa kwenye mchakato wa kuweka uzio kuzunguka kiwanja hicho, na cha ajabu ni kwamba, alikuwa akifanya hivyo usiku huku akiongozana na mabaunsa wenye mapanga," alidai.

Wakazi wa eneo hilo walidai viongozi wao wamekuwa wakishirikiana na wawekezaji wasio waaminifu kuuziana ardhi iliyotengwa kwa shughuli za burudani kinyume cha sheria.

Waliiomba serikali kuingilia kati suala hilo kwa kubatilisha umiliki wa eneo hilo kwa kuwa hawakushirikishwa katika kuuzwa kwake.

## Mkurugenzi IPTL aunganishwa kesi ya kina Lugemalira

Na Hellen Mwango

KAIMU Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL), Joseph Makandege, ameunganishwa katika kesi na Mfanyabiashara Harbinder Sethi na mwenzake akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha Dola za Marekani 980,000.

Makandege amefanya idadi ya washtakiwa katika kesi hiyo kufika watatu na idadi ya mashtaka kufika 15 kutoka 12 ya awali.

Kigogo huyo ambaye pia ni Wakili wa Kujitegemea, alisomewa mashtaka matano ya kula njama, kuratibu genge la uhalifu, kujipatia na kutakatisha fedha, mbele ya Hakimu Mkazi Thomas Simba wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Jopo la Upande wa Jamhuri likiongozwa Mawakili wa Serikali Wakuu, Paul Kadushi, Faraja Nchimbi na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon.

Kadushi alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi, 2014, mahali tofauti jijini Dar es Salaam, Sethi, Makandege na James Lugemarila walikula njama ya kutenda kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku ya tukio la kwanza, washtakiwa wote watatu, waliratibu genge la uhalifu kwa lengo la kujinufaisha wao wenyewe binafsi.

Nchimbi alidai Makandege anakabiliwa na shtaka la 13, kwamba kati ya Januari 23 na Februari 10, 2014, katika Benki ya Stanbic tawi la Centre lililoko Kinondoni na Benki ya UBL (T) Ltd iliyoko Ilala, mshtakiwa alijipatia kwa njia ya udanganyifu, Dola za Marekani 380,000 na 600,000.

Katika shtaka la 14, Upande wa Jamhuri ulidai kuwa katika benki za Stanbic na UBL, Makandege aliisababishia Serikali ya Jamhuri ya Muungano hasara ya Dola za Marekani 980,000.

Wankyo alidai katika shtaka la 15, siku na tarehe ya tukio la 13, Makandege alitakatisha Dola za Marekani 980,000 wakati akijua ni zao la genge la uhalifu.

Mshtakiwa huyo hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za ujumumu uchumi.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na uliomba tarehe nyingine ya kutajwa na kumuunganisha mshtakiwa na wenzake.

Hakimu Simba alisema kesi hiyo itatajwa Januari 2, mwakani, mshtakiwa apelekwe mahabusu.

Katika kesi hiyo, Sethi na Lugemarila walifikishwa mahakamani hapo mapema 2017 wakikabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya kula njama na kutakatisha Sh. bilioni 309 na Dola za Marekani 22,198,544.6, mali ya Serikali ya Tanzania.




Meneja Mwandamizi wa Idara ya Kadi Benki ya NMB, Manfredy Kayala, akimkabidhi zawadi ya simu mpya aina ya Tecno Pop 2 dereva wa Bodaboda kituo cha Buguruni Rozana, Mohamed Abdallah, baada ya kuibuka mshindi wa kufanya mialama ya kibenki zaidi ya 200 kwa mwezi kulipwa nauli na abiria wake kwa kutumia huduma mpya ya Master Boda QR, wakati wa hafla fupi ya kukabidhi zawadi za washindi iliyofanyika Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam, jana. Kulia ni `Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Bodaboda na Bajaji Mkoa wa Dar es Salaam, Michael Massawe.

# RC atishia kushtaki wabunge

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, amesikitishwa na baadhi ya wabunge wa mkoa huo kutoshiriki vikao na shughuli mbalimbali za kiserikali bila kutoa taarifa.

Amesema endapo hawatabadilika, atawafikishia ujumbe kwa wananchi waliowachagua ili wachukue hatua.

Ole Sanare aliyasema hayo katika kikao cha Bodi ya Barabara na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) mjini hapa, akieleza kuwa ni muhimu wabunge kushiriki vikao hivyo vikiwamo vya maandalizi ya bajeti ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Hivi ikitokea katika bajeti ijayo wakakosa fedha za miradi ya maendeleo, itakuwaje? Uwapo wao katika vikao hivi ungesaidia kutoa ushauri wa kuboresha mapendekezo yanayowasilishwa na watalaamu ili kusaidia miradi iliyopo katika maeneo yao kupata fedha," alisema.

Alibainisha kuwa mkoa huo una idadi ya wabunge 14, lakini walioudhuria vikao hivyo ni wanne tu bila kuwapo kwa taarifa za wabunge wengine 10 ambao hawakuonekana.

Alisema katika kikao cha awali cha kujadili maendeleo ya elimu, mahudhurio ya wabunge wa mkoa huo pia hayakuwa mazuri huku wakitambua kuwa suala hilo linawagusa watoto wa wapigakura wao.

Mkuu wa Mkoa huyo pia aliweka wazi kuwa hata wakati wa ziara zake za kujitambulisha katika wilaya za mkoa huo baada ya kuteueliwa na Rais John Magufuli hivi karibuni, baadhi ya wabunge hawakuonekana na badala yake alikutana na wananchi na watendaji wa serikali katika maeneo hayo.

Alisema kuwa yapo baadhi ya maeneo wananchi wanalia na kulalamika kutowaona wabunge wao kwa muda mrefu na hivyo kushindwa kuwasilisha kero zao.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Emanuel Kalobero, alisema vikao hivyo vilisogezwa mbele ili kutoa fursa kwa wabunge kushiriki vikao.

Akizungumzia kauli ya mkuu wa mkoa kuhusu wabunge kutohudhuria vikao hivyo, Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi Morogoro, Maulidi Ibangi, alidai inatokana na kutokuwapo sheria inayowabana watunga sheria kuwajibika kwa wapigakura wao.

"Kwa kuwa hakuna sheria inayobana kuwajibika kwa wananchi wao, vikao kama hivi vya kujadili maendeleo ya mkoa hawavipi umuhimu wowote na hilo si kwa wabunge wa vyama vya upinzani tu, bali ni hata na wale wa chama tawala," alidai.

# Wasiojulikana wadaiwa kumteka ofisa wa LHRC

**Na Salome Kitomari**

OFISA wa Kitengo cha Elimu kwa Umma wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti, anadaiwa kutekwa na watu wasiojulikana akiwa eneo la Mwenge wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii na baadaye jana kuthibitishwa na LHRC, Magoti anadaiwa kutekwa na watu watano wasiojulikana mara tu baada ya kuteremka kwenye pikikipi akiwa eneo hilo jana asubuhi.

"Tumepokea taarifa za kuhuzunisha kwamba ofisa wetu Kitengo cha Elimu kwa Umma, ametekwa na watu waliovalia mavazi ya kiraia maeneo ya Mwenge jijini Dar es Salaam. Tunaendelea kufuatilia taarifa hizi na tutatoa taarifa zaidi," LHRC ilieleza katika ukurasa wake rasmi wa Twitter jana.

Kamanda wa Polisi Polisi Mkoa wa Kinondoni, Mussa Taibu, alipotafutwa na Nipashe jana mchana, alikataa kuzungumzia suala hilo kwa madai kuwa alikuwa kwenye kikao.

Pia, simu ya Kanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Larazo Mambosasa, ilikuwa inaita pasi na kupokewa alipotafutwa na gazeti hili jana.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), katika tamko lake kuhusu taarifa za kutekwa kwa ofisa huyo, ulidai kuwa Magoti alichukuliwa na watu watano akiwa kwenye kituo cha mafuta cha Puma kilichoko Mwenge, kisha kuondoka naye kwenda kusikojulikana.

"Tukio hilo lililotokea asubuhi ya leo (jana), watu hao walitumia nguvu kumuingiza Tito kwenye gari aina ya Toyota Harrier wakiwa wamevalia mavazi ya kiraia. Jitihada za kumtafuta katika vituo mbalimbali vya polisi zinaendelea.

"Tunaliomba Jeshi la Polisi kuchukua hatua za haraka na za makusudi kuhakikisha mtetezi huyu anapatikana akiwa salama," THRDC waliomba katika taarifa yao hiyo. Mkurugenzi wa LHRC, Anna Henga, pia alitumia ukurasa wake wa Twitter kutoa taarifa ya kutoweka kwa ofisa huyo akisema: "Mfanyakazi wa LHRC Tito Magoti ametoweka leo (jana) asubuhi kwa kutekwa na watu wasiojulikana maeneo ya Mwenge, Dar es Salaam."

Nipashe ilizungumza na mkurugenzi huyo na akadai kuwa wamemtafuta kwenye vituo vyote vya polisi jijini bila mafanikio na walichojibiwa ni kwamba hajakamatwa na polisi na ndiyo maana hayupo kwenye vituo vyao.

Alidai wamewasiliana na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, ambaye amewapa ushirikiano mkubwa na sasa wanawasiliana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, na wamefungua jalada kwenye Kituo cha Polisi Mabatini, Kinondoni jijini.

Alidai ofisa huyo ni "mwanaharakati 'active' kwenye mitandao ya kijamii kwa kutetea watu wengi kupitia ukurasa wake".

Katibu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, katika taarifa yake jana, alisema wamepokea kwa huzuni taarifa za kutekwa kwa mwanasheria na mwanaharakati huyo na kwamba wamewasiliana na Jeshi la Polisi ambalo limekana kumshikilia. "Kauli hii inaashiria kurejea upya kwa utamaduni wa watu wasiojulikana kuwateka wanaharakati, waandishi wa habari na watu wengine.

"Tunawataka polisi kuhakikisha anarejeshwa haraka akiwa hai, tunaamini polisi wakiamua wanaweza kumrejesha mara moja na kuwakamata waliomteka," alidai.


SHIRIKA LA UMEME TANZANIA

TANESCO
We light up your life

TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lina watangazia wateja wake wote zikiwemo Taasisi za Serikali na binafsi, Mashirika ya umma, Viwanda na watu binafsi wenye madeni ya bili za umeme kuwa;

TANESCO inaendesha zoezi maalum la kusitisha huduma ya umeme kwa wateja wote wanaodaiwa bili za umeme.

Wateja wote wenye madeni wanatakiwa kulipa bili zao haraka ili kuepuka adha ya kusitishiwa huduma ya umeme katika msimu wa sikukuu.

TANESCO HAITATOA TAARIFA NYINGINE ZAIDI YA TANGAZO HILI.

Imetolewa Na:
OFISI YA UHUSIANO
TANESCO MAKAO MAKUU
18 Disemba2019

# TCC yapongezwa kusaidia wanawake wenye ulemavu

**Na Moshi Lusonzo**

WABUNGE wameipongeza Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC) kwa msaada wa Sh. milioni 20 za kuanzisha kiwanda cha ushonaji kwa ajili ya wanawake wenye ulemavu Wilaya ya Temeke. Wakizungumza katika hafla ya kukabidhi hundi iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam, Mbunge wa Temeke, Abdallah Mtolea na wa Viti Maalum, Mariam Kisangi, walisema kampuni hiyo imeunga mkono kwa vitendo kauli ya Rais John Magufuli, kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Msaada huo walikabidhiwa Wanawake Wenye Ulemavu wa Viungo (Uwaviute) na utahusisha ununuzi wa vyerehani 30, malighafi, vifaa mbalimbali na pango la jengo kwa muda wa mwaka mmoja.

Mtolea alisema fedha hizo ambazo TCC imetoa, ni kichocheo cha kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla kutokana na uzalishaji utakaofanyika utaongeza ajira.

"Nawapongeza TCC kwa kufanya jambo hili kubwa kwani kusaidia wanawake walemavu kwa kuwapa mtaji wa uzalishaji ni njia bora ya kuwafanya wajitegemee kuliko kubaki wakiomba," alisema Mtolea.

Alisema amewapigania hadi kupewa mtaji huo, hivyo kilichobaki kwa wanakikundi hao ni kulipa kwa kuzalisha bidhaa na kupata faida.

Naye Kisangi alisema jamii inatakiwa kuwa na mtazamo mpya kwa watu wanaoishi na ulemavu kwani watu hao wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi na kuhudumia familia zao kama walivyo wengine.

Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa TCC, Godson Kiliza, alisema taasisi yake imeweka utaratibu wa kusaidia watu wenye ulemavu nchi nzima na kwa Temeke wameamua kuongeza nguvu kwa kuwasaidia kiuchumi na kulinda mazingira.

Amesema hivi karibuni wamesambaza mapipa ya ukusanyaji wa taka 241 katika mitaa tofauti na kila mwezi wamepanga kuongeza mapipa 50.

"Pamoja na juhudi hizo tunapenda kusema kuwa TCC itaanza kutoa msaada wa vifaa mwendo 320 ikiwamo baiskeli, viti, magongo na fimbo nyeupe kwa walemavu wanaoishi Temeke na Mbagala," alisema Kiliza. Naye Meneja Uhusiano, Emma Uriyo, aliwataka wanakikundi kutunza mashine na kufanya kazi kwa bidii, ili kuonesha jamii kwamba watu wenye ulemavu wakiwezeshwa wanaweza.

Aliwataka wadau wengine kujitokeza kuliangalia kundi hilo kwa lengo la kuwatoa katika unyonge na kuwakwamua kiuchumi.



Meneja Mwandamizi wa Idara ya Kadi Benki ya NMB, Manfredy Kayala, akimkabidhi zawadi ya simu mpya aina ya Tecno Pop 2 dereva wa Bodaboda kituo cha Buguruni Rozana, Mohamed Abdallah, baada ya kuibuka mshindi wa kufanya mialama ya kibenki zaidi ya 200 kwa mwezi kulipwa nauli na abiria wake kwa kutumia huduma mpya ya Master Boda QR, wakati wa hafla fupi ya kukabidhi zawadi za washindi iliyofanyika Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam, jana. Kulia ni Meneja Mwandamizi wa Idara ya Bidhaa za Kadi, Lupia Matta na Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Bodaboda na Bajaji Mkoa wa Dar es Salaam, Michael Massawe.

# Ujenzi bandari ya Rukwa wanoga

**Na Elizabeth Zaya,** RUKWA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA), imefikia asilimia 85 ya ujenzi wa bandari ndogo ya Kabwe wilayani Nkasi mkoani Rukwa.

Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Percival Salama, aliyasema hayo wakati akizungumza na wandishi wa habari katika ziara ya kuangalia shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na TPA.

Salama alisema bandari hiyo ni ya kisasa na itakuwa ya pili kwa ukubwa kwa mkoa huo baada ya Bandari ya Kasanga na kwamba itakuwa mkombozi wa usafiri wa maji katika ziwa hilo.

Mhandisi wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Nyakato Lwamnana, alisema Bandari ya Kabwe ni kitovu cha biashara kati ya Mkoa wa Rukwa na mikoa mingine pamoja na nchi jirani. "Bandari hii ina umuhimu mkubwa kwa ustawi wa uchumi Tanzania. Uboreshaji wa bandari hii ni wa miezi 24 na unatarajiwa kumamilika mwishoni mwa Machi mwakani ukitumia zaidi ya Sh. bilioni saba," alisema.

Alibainisha kuwa mradi huo unahusisha ujenzi wa gati lenye urefu wa mita 74 kuingia majini, jengo la abiria, ghala, nyumba za watumishi, jengo la mgahawa na uzio utakaozunguka eneo lote la bandari pamoja na ujenzi wa barabara ya mita 600 kutoka eneo la bandari hadi nje ya bandari hiyo.

Alisema mradi huo ukikamilika, utaongeza ufanisi wa huduma za bandari hiyo na kuingiza mapato zaidi.

Mwakilishi wa Kampuni ya Summry inayotengeneza bandari hiyo, William Shila, alisema miongoni mwa vikwazo walivyokumbana navyo wakati wa ujenzi wa bandari hiyo, ni uwapo wa mchanga mwingi katika eneo hilo.

"Na katika kipindi hiki chote tunachojenga, tumekuwa tukipata wageni tofauti na wengine huwa wanajitambulisha kuwa ni wafanyabiashara kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huwa wanatuuliza kwamba tunamaliza lini ujenzi.

"Na wanasema njia hii itakuwa fupi kwao kusafirisha mizigo yao, na ndiyo maana pamoja na vikwazo tunavyokutana navyo, tunapambana kuhakikisha tunamaliza kwa wakati ili tuwakabidhi TPA na shughuli zao ziendelee," alisema.

## Wachimbaji wapewa angalizo la kemikali

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

MKUU wa Wilaya ya Geita, Josephat Maganga, amewataka wachimbaji na wachenjuaji wa dhahabu mkoani Geita, kuzingatia taratibu na matumizi salama ya kemikali na watakaokwenda kinyume watachukuliwa hatua za kisheria.

Maganga aliyasema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya matumizi salama ya kemikali kwa wachimbaji na wachenjuaji wa dhahabu mkoani humo yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) Kanda ya Ziwa.

"Najua mmejifunza mengi na mmepata uelewa wa kutosha ili mkienda kwenye shughuli zenu za uchimbaji, mkatekeleze kwa vitendo elimu hii mliyoipata ili kulinda afya za wananchi na mazingira.

"Tukigundua umepata elimu hii na hautekelezi kwa vitendo, basi tutakuchukulia hatua kwa sheria tulizonazo, mnatakiwa kutambua pamoja na kupata fedha kutokana na uchimbaji wa madini, ni muhimu kulinda afya za wananchi kutokana na matumizi yasiyo salama ya kemikali ambazo nyie wataalamu mnatakiwa kuzisimamia," aliagiza.

Aliwataka waliopata mafunzo hayo kuwa mabalozi kwa wachimbaji ambao hawakuhudhuria mafunzo ili kusaidia kupunguza madhara yanayosababishwa na kemikali zisipotumika vizuri katika shughuli zao.

"Msifunge mdomo mnapotoka hapa kwenda kwenye maeneo yenu ya uchimbaji, bali muwe mabalozi kwa kupeleka habari njema ya matumizi salama ya kemikali kwa wenzenu.

"Elimu mliyoipata mkaitumie kupunguza na kuondoa upungufu uliopo kwenye maeneo ya kazi na hivyo kulinda afya zenu, jamii inayowazunguka na mazingira na ukipata tatizo katika matumizi ya kemikali, usisite kuwasiliana na wahusika ili kupata msaada," alishauri.

Awali Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, alisema GCLA itaendelea kutoa mafunzo kwa wachimbaji wa madini na kufungua ofisi katika Mkoa wa Geita ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

"Washiriki wa mafunzo wametupa hamasa kubwa ya kutoa mafunzo ya namna hii mara kwa mara kwa lengo la kusaidia kuongeza uelewa wa matumizi salama ya kemikali katika shughuli za uchenjuaji.

"Pamoja na utoaji wa mafunzo, mamlaka ina mpango wa kuanzisha ofisi ndogo ya Geita ili kusogeza huduma karibu na wananchi na jamii ya wachimbaji wa dhahabu," aliahidi.

Washiriki 78 walipatiwa mafunzo na kukabidhiwa vyeti baada ya kukamilisha mafunzo hayo.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, akiwapa Vitambulisho vya Bima ya Afya baadhi ya wakazi wa Mkoa huo ambao wamefanikiwa kujiunga na mpango wa vifurushi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mafanikio 11 Hospitali Rufani Mbeya miaka minne ya JPM

**Na Mwandishi wetu,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), imetaja mafanikio 11 iliyoyapata katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha maji tiba lita 3,840 kwa mwezi.

Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, alibainisha mafanikio hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Alisema hospitali hiyo imetekeleza kwa vitendo sera ya viwanda na maagizo ya Rais John Magufuli kwa kuanzisha kiwanda cha uzalishaji wa maji tiba.

Alisema kiwanda hicho kilianzishwa Februari mwaka huu, ujenzi wake ukigharimu Sh. milioni 120 kwa mapato ya ndani na kinazalisha maji tiba yenye mita za ujazo 250 na kwamba 500 zimeanza kutumika kuhudumia wagonjwa wenye uhitaji.

"Hali hii imesaidia kuondokana na adha ya kununua au kuagiza dripu nje ya nchi, na kiwanda kina uwezo wa kutengeneza maji tiba lita 3,840 kwa mwezi, mahitaji ya hospitali ni lita 5,232 na hivyo kukidhi kwa asilimia 73 ya uhitaji wa maji tiba kwa ajili ya hospitali," alisema.

INAENDELEA UK. 8

# Takukuru yatoa neno kwa wanawake rushwa ngono

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, ametoa wito kwa wanawake kutoa taarifa za kuombwa rushwa ya ngono, akisisitiza kuwa inadhalilisha utu wa kundi hilo.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana kiongozi huyo wa Takukuru alisema taasisi hiyo imejipanga vyema kukabiliana na vitendo vya rushwa ya ngono.

Alisema kitendo hicho ni cha aibu na kamwe taasisi hiyo haitakifumbiwa macho.

"Rushwa ya ngono haimsaidii yeyote, zaidi itakuwa inamdhalilisha mwanamke, tunatoa wito kwa wanawake kutoa ushirikiano pale wanapokumbana na tatizo hili, tuko tayari kushirkikiana nao," alisema.

Aliwataka wanafunzi walioko katika shule na vyuo mbalimbali nchinio kuepuka vitendo hivyo kwa kuwa vinashusha hadhi na kudhalilisha kutu wao.

Suzana aliwataka wanafunzi waiarifu taasisi hiyo wanapoona wanasumbuliwa na walimu kwa kuwaomba rushwa ya ngono ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Vitendo vya rushwa ya ngono vimeendelea kuripotiwa katika maeneo mbalimbali nchini. Hivi karibuni kuliibuliwa kashfa hiyo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), baadhi ya wahadhiri wake wakituhumiwa kuomba rushwa kwa wanafunzi ili kuwafaulisha.

Pia, katika mahafali ya Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) mwaka huu, uongozi wa chuo hicho ulimweleza Rais John Magufuli kuwa unakabiliwa na tatizo hilo kwa baadhi ya wanafunzi kuombwa rushwa na wahadhiri na wanafunzi kuwataka wahadhiri kingono ili kutengeneza mazingira ya kufaulishwa.

Kadhia hiyo imeripotiwa katika vituo vya afya, baadhi ya wauguzi na madaktari wakituhumiwa kuomba rushwa kwa wagonjwa kama sehemu ya malipo ili kuwapatia matibabu.

# Mwasisi chama cha wafanyakazi afariki

**Na Maulid Mmbaga**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa kwanza wa chama cha wafanyakazi nchini, Nekamia Kazimoto, amefariki dunia.

Kazimoto alifariki dunia juzi akiwa nyumbani kwake, Kayanga, Karagwe mkoani Kagera.

Kazimoto aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Mashamba ya Miwa.

Aidha, amewahi kuandika vitabu mbalimbali ikiwamo kitabu kiitwacho 'Maisha na Harakati za Kazimoto'.

Akizungumza na gazeti letu kwa njia ya simu, mtoto wa marehemu, Florence, alithibitisha kutokea kwa msiba huo na kwamba mazishi yatafanyika keshokutwa.

"Familia imepata pigo kubwa kwa kutokwa na mpendwa wetu kwani alikuwa kiongozi aliyetuongoza na kutushauri mambo mbalimbali yakifamilia," alisema.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, klabu zitupie jicho mikataba hii ya mkopo

**KWA** sasa klabu za Tanzania zipo katika harakati za kuimarisha vikosi vyao, baada ya usajili wa dirisha dogo kufunguliwa rasmi kwa Tanzania Bara na hata ule wa visiwani Zanzibar.

Kwa Tanzania Bara, dirisha dogo lilifunguliwa tangu Desemba 16 na linatarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani, wakati lile la Zanzibar likifunguliwa siku tano kabla na likitarajiwa kufungwa Januari 9, mwakani.

Kwanza ni uwanja mpana kwa klabu za Ligi Kuu Bara na Zanzibar pamoja na zile za Ligi Daraja la Kwanza na la Pili kuweza kutafuta wachezaji kuanzia Bara hadi visiwani kwa pande zote ili kuimarisha vikosi vyao kwa kuwa madirisha yote yapo wazi kwa sasa.

Tunatambua kufunguliwa kwa dirisha hilo ni nafasi pekee kwa klabu hususan kuweza kuboresha idara ambazo zilikuwa zimepwaya ama kuandamwa na majeruhi ili kuweza kujiimarisha kwa raundi ya pili ya ligi hiyo. Aidha, Nipashe linafahamu katika dirisha hili wapo baadhi ya wachezaji watatemwa ili kutoa nafasi kwa nyota wapya ambao klabu husika zinaamini wanaweza kuzisaidia kutimiza malengo yao, lakini pia wapo walikuwa wanacheza kwa mkopo klabu zao zitahitaji kuwarejesha huku wengine wakitolewa kwa mkopo pia.

Hata hivyo, wakati huu harakati hizo za usajili zikiendelea kwa wachezaji kutoka klabu moja hadi nyingine, kumeanza kufurukuta mvutano kwa baadhi ya klabu kutokana na mikataba yao na wachezaji waliowatoa kwa mkopo kutokuwa na vipengele muhimu vinavyoweka mambo yote wazi.

Kwa siku takriban nne sasa, kumeibuka mvutano mkubwa kati ya Azam FC na Klabu ya Polisi Tanzania kuhusu mkataba wa mshambuliaji Ditram Nchimbi, anayedaiwa kupata baraka kutoka kwa klabu yake mama kusajiliwa na Yanga.

Kama ilivyo na inavyofahamika kwa klabu hizo mbili, ni kwamba Nchimbi alikuwa akiichezea Polisi Tanzania kwa mkataba wa mkopo akitokea Azam FC, ambao unaelezwa ulikuwa wa msimu mzima. Kwa mujibu wa Polisi Tanzania walikubaliana na Azam kumtumia mchezaji huyo hadi mwishoni mwa msimu ndipo arejee klabuni kwake, na hapakuwa na kipengele chochote kinachoiruhusu Azam kumchukua katikati ya msimu, jambo ambalo linawafanya kupaza sauti za kumzuia kuuzwa Yanga.

Na kwa upande wa Azam FC inaeleza kwamba hapakuwa na kipengele chochote kinachoeleza kwamba hawataruhusiwa kumchukua mchezaji wao watakapomhitaji, huku wakiamini ni sawa na mtu kumpa mtoto wako akulelee, hivyo unapomhitaji unaweza kumchukua wakati wowote.


Azam pia, inaeleza baada ya Yanga kufika dau la kumnunua Nchimbi, ilitoa kipaumbele kwa Polisi Tanzania kama inamhitaji jumla imnunue, lakini ikawaeleza haina uwezo huo na kuwaruhusu kuendelea na taratibu zingine za kumuuza.

Kwa ujumla, Nipashe tumefuatilia kwa kina mvutano uliopo kwa klabu hizo mbili na kubaini kuna utata mkubwa na kutokuwepo kwa uwazi wa mikataba ya wachezaji wanaotolewa kwa mkopo kutoka klabu moja hadi nyingine. Tunatambua mikataba ya mikopo kwa wachezaji huwa ina vipengele vingi muhimu na hawatolewi kiholela kama ambavyo klabu zetu nchini zinavyofanya, kwani; awali kabisani lazima mkopo huo uainishe wazi ni wa muda gani na nani hasa atamlipa mshahara mchezaji husika.

Pili mkataba wa mkopo unaweza kuwa na kipengele kwa klabu mama kumhitaji mchezaji wao muda wowote ama hataruhusiwa kucheza dhidi ya klabu yake hiyo pindi timu hizo zitakapokutana, lakini pia pindi itakapotaka kumuuza klabu anayoichezea kwa mkopo ipewe nafasi ya kwanza kumnunua na ikishindindwa ama kutohitaji tena huduma yake ndipo auzwe kwingineko.

Hayo ni machache tu katika mengi yanayopaswa kuwekwa wazi katika mikataba ya wachezaji wanaotolewa kwa mkopo, hivyo, Shirikisho la Soka nchini (TFF) na klabu kuna haja ya kukaa chini na kunyoosha mambo kwa kuhakikisha vipengele hivyo muhimu vinakuwepo ili kuepuka mivutano kama hii inayoendelea kwa Azam FC na Polisi Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kila king'aacho si dhahabu

Na Barnabas Maro

**KIGAE** cha chupa kikiwa juani hung'aa. Hivyo isidhaniwe ni dhahabu inayochimbwa ardhini baada ya utafiti na kugundua uwapo wa madini hayo.

Hakuna madini yanayopatikana kirahisi. Mpaka kupata madini ya aina yoyote, watu hutoka jasho na wengine kupoteza maisha mpaka kuyapata. Hata yanapopatikana huwa na kazi ya kuyasafisha na kuyatayarisha ili kuyapeleka sokoni.

Wahenga walisema: "Sihadaike na rangi, sifa ya chai ni sukari." Maana yake usidanganyike kutokana na rangi ya chai, utamu wake hutokana na sukari.

Methali hii hutumiwa kumkanya mtu asipumbazike au asivutwe na sifa za nje za kitu ila akichunguze kwa ndani.

Dirisha dogo la usajili wa wacheza kandanda lilifunguliwa rasmi nchini wakati nikiandaa makala haya. Kila timu, Simba imekuwa mbioni kufanya usajili wakati watani zao, Yanga tayari washasajili, lengo likiwa ni kujaza nafasi za wachezaji walioachwa, majeruhi au walioomba kuondoka baada ya kuona hawapati nafasi ya kucheza.

Halahala Simba na Yanga kukurupukia usajili mdogo au mkubwa. Mara nyingi imeonekana kuwa mwafanya hivyo kupimana uwezo wa fedha na umaarufu badala ya kuwapata wachezaji mahiri.

Matokeo yake, baadhi ya wachezaji hukosa nafasi kwenye kikosi cha kwanza na kuwekwa benchi kwa muda mrefu! Usajili haufanywi kwa papara (ukosefu wa umakini katika kufanya jambo) au kushindana na timu nyingine.

Hapa ndipo pa kujiuliza: Hao wanaowasajili wachezaji kisha kukosa nafasi za kucheza, kilichowavutia hata kuwasajili ni kitu gani? Timu zinazosajili wachezaji kuanzia wanne mpaka kumi maana yake ni kuwa wachezaji wote waliopo nchini hawafai! Si kweli.

Tatizo ni baadhi ya viongozi wa Simba na Yanga kuingilia kazi ya makocha (walimu) katika usajili. Hufanya hivyo ili wasajiliwe wachezaji watakaokubaliana nao kugawana sehemu ya fedha wanazotaka kabla ya kusajiliwa!

Wahenga hawakukosea walipo sema "Fedha fedheha." Maana yake pesa huweza kuleta mambo ya aibu baina ya binadamu. Hutumiwa kutuonya kuhusu maovu yanayoweza kusababishwa na pesa.

Usajili ni kazi ya mwalimu baada ya kuona eneo fulani linahitaji mchezaji mbadala au msaidizi wa aliyepo. Endapo mchezaji aliyependekezwa na mwalimu ili asajiliwe kisha kutompanga kwa kutokuwa na sifa zitakiwazo, ni wajibu wa uongozi kumhoji kwa nini imekuwa hivyo.

Wachezaji hawatafutwi haraka haraka kama watu wachaguavyo nguo za mitumba. Wanaweza kufutiliwa hata kwa mwaka mzima na zaidi, hasa wale wenye umri mdogo.

Hili laweza kufanyika kwa mafanikio kama klabu zitakuwa na timu za vijana watakaoandaliwa kuchukua nafasi za wakubwa watakaohitajika na timu zingine za ndani au nje ya nchi.

Tofauti na hili, klabu zetu zitakuwa zikitegemea wachezaji wa kigeni zaidi na kusababisha nchi kutokuwa na timu nzuri za taifa.

Jambo lingine ni klabu kuwa na viwanja vyao vya mazoezi na mashindano. Viwanja hivyo viwe na mahitaji yote muhimu kwa wachezaji: ukumbi wa michezo ya mazoezi ya viungo (gym), bwawa la kuogelea, zahanati, bwalo la kulia chakula, chumba maalum cha mafunzo ya ubaoni n.k.

Kadhalika, kuwe na vyumba vya kulala timu zitakapokuwa kambini kujiandaa na michezo ya mashindano badala ya kupanga kwenye hoteli kubwa na kulipa hela nyingi. Ikumbukwe kuwa kupanga ni kuchagua.

Yasikitisha kuwa viwanja vingi humu nchini vyaitwa 'viwanja' lakini kiukweli havistahiki kuitwa hivyo kwa jinsi vilivyochakaa.

Chama Cha Mapinduzi kimetwaa takriban viwanja vyote vikubwa vya kandanda nchini, lakini kimeshidwa kabisa kuviendeleza ila huvipamba kwa rangi zake tu! Kama kimeshindwa kuviendeleza na kuvitunza, basi vikabidhiwe kwa mamlaka za miji na majiji.

Wakati hayo yakifanyika, timu zinazoshiriki Ligi Kuu zishauriwe kuwa na viwanja vyao badala ya kutegemea vya wenzao au vya taifa. Azam FC imeweza hilo na sasa Simba nayo imefikia hatua hiyo.

Wale jamaa wa Jangwani (Yanga) walipewa uwanja kule Kigamboni jijini Dar es Salaam. Aliyewapa ni mpenzi kindakindaki (halisi) wa Simba, Paulo Makonda aliye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Yanga wasilaze damu kwani muda haumsubiri mtu. Ilisemwa na wahenga kuwa "Ngoja ngoja huumiza matumbo." Maana yake kuambiwa "ngoja ngoja" kwa kuwa chakula kinaletwa huishia kuyaumiza matumbo kwa njaa.

Methali hii huweza kutumiwa na mtu anayeonesha kucheleachelea (-wa na hofu ya; -wa na wasiwasi wa) katika kufanya jambo kwani ni tabia inayoweza kumletea madhara baadaye. Methali hii inamhimiza mtu kutenda jambo alilokusudia.

HABARI KITAIFA

# Madereva Uber watishia kufanya uamuzi mgumu

**Na Enock Charles**

CHAMA cha madereva wanaosafirisha abiria kwa njia ya mtandao (Tada), kimewataka wamiliki wa kampuni za huduma za usafiri kukutana ili kutatua matatizo ya usafirishaji yaliyopo baina ya madereva hao na kampuni hizo.

Usafiri huo unahusisha taksi za 'Uber na Taxify'ambazo wateja wanawasiliana nao kwa njia za simu baada ya kuangalia taarifa kwenye mtandao.

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa Tado, Linus Chuwa, alisema tangu kuanzishwa kwa usafirishaji kwa njia ya mtandao madereva na wamiliki wa vyombo vya usafiri vivyotumika na mitandao hiyo hasa Uber na Taxify hawajawahi kukaa pamoja, kupanga bei au asilimia za mapato.

"Tuna mambo mawili ambayo tutayafanya, kwanza tumetoa siku saba wakutane nasi kutatua changamoto hizo na tumeshawaandikia barua, pili kama ikishindikana tutaenda mahakamani " Chuwa alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya usuluhishi ya chama hicho Ebony Ford, alisema kampuni hizo wakati zinaanzishwa nchini bei ilikuwa Sh.950 kwa kilometa na 150 kwa dakika ya safari tofauti na sasa ambapo bei imekuwa ni Sh.450 kwa kilometa na Sh.80 kwa kila dakika ya safari jambo alilodai ni gharama kubwa za uendeshaji kwa madereva na hivyo huambulia kipato duni.

"Wao ndiyo wapangaji wa bei na wakusanyaji wa mapato hizo asilimia 25 za Uber au 20 za Taxify hazijawahi kupangwa na madereva au wamiliki wa chombo lakini sisi tunaona ni kubwa sana na za kuwakandamiza madereva " Ford alisema

Mwenyekiti huyo aliiomba serikali kuingilia kati suala hilo kwa kile alichoeleza kuwa hakuna bei elekezi kitu alichodai kusababisha kampuni hizo kujipangia bei kwa manufaa yao bila kujali maslahi ya madereva hao .

Alilalamikia pia 'ofa na promosheni' zinazotolewa kwa wateja na kampuni hizo kwa madai kuwa zinamgharimu dereva na hivyo kusababisha mara nyingine kuzuka kwa ugomvi baina ya abiria na madereva wa vyombo hivyo baada ya kutofautiana katika suala la bei.

Gazeti hili liliwatafuta wamiliki wa mitandao hiyo, uber ilimtaka mwandishi kuandika maswali na kuyatuma katika mtandao wake, hata hivyo hayakujibiwa hadi gazeti hili linakwenda mitamboni huku kwa upande taxify simu yao ikiita bila kupokelewa.

# Taasisi zatakiwa kufundisha kutumia akili kubuni mambo

**Na Mary Geofrey**

TAASISI za elimu zikiwamo shule na vyuo, zimeshauriwa kuanza kutoa elimu inayowezesha wanafunzi kutumia akili , kubuni na kuanzisha mambo yanayoleta mabadiliko katika maisha yake na ya jamii.

Rai hiyo, ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mjasiriamali, Erick Shigongo, wakati akizungumza katika hafla ya kumkabidhi hundi ya Sh. milioni 10 mshindi wa shindano la Mamakasema, kujifunza Ni mtaji, lililoandaliwa na kampuni ya teknolojia ya fedha ya Nala.

Katika shindano lililohusisha watumiaji wa huduma ya Nala zaidi ya 2,000 Samuel Kisinga kutoka mkoa wa Ruvuma aliyejishindia kitita hicho.

"Nimefurahi sana kuona kuna vipaji vingi vya vijana vinaibuka zaidi. Naomba Watanzania wawaunge mkono vijana ambao wanatumia akili zao kubuni mbinu mbalimbali za kutafuta suluhisho la kudumu la matatizo," alisema Shigongo na kuongeza "Vyuo vikuu na shule zihakikishe zinafundisha wanafunzi kutumia akili zao kutafuta suluhisho la changamoto zinazoikabili jamii la sivyo tutaendelea kuwa na lundo la wanafunzi wenye elimu kubwa wasiyo na akili za kutatua mambo."

Mkurugenzi Mtendaji wa Nala, Benjamin Fernandes, alisema baada ya kufanikiwa kutoa huduma ya suluhisho la mawasiliano kupitia Nala, waliona faida hiyo warudishe kwa jamii ambayo ni vijana wanaonzisha miradi mbalimbali ya kujikwamua kiuchumi.

"Nala ilianzisha shindano la Mamakasema, kujifunza ni mtaji ambalo lilikuwa na dhumuni la kumsaidia mjasiriamali mmoja mwenye biashara au anayehitaji kuanza biashara," alisema Fernandes.

Alisema kupitia shindano hilo mshindi aliyejishindia mtaji wa Sh. milioni 10 pia atapata mafunzo ya namna ya kukuza na kuendesha biashara kutoka Nala.

Aidha, mshindi Samuel Kisinga, akizungumzia biashara zake, alisema anajihusisha na kutunza mazingira, kukusanya na kutumia takataka zilizozagaa mtaani zikiwamo (ceiling board) na gypsum kutengeneza mapambo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akisikiliza maelezo ya mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Chiungutwa, Masasi. Kituo hicho bado hakijakamilika kwa wakati baada ya vifaa mbalimbali zikiwamo nondo 200 kuibwa. Jafo alifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo jana wilayani Masasi. **PICHA: HAMISI NASIR**

# Elimu zaidi itolewe faida nishati jadidifu

**Na Mary Geofrey**

KATIKA jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, wadau wa mazingira wametaka wananchi waelimishwe zaidi umuhimu na faida za kutumia nishati jadilifu (renewable energy).

Aidha wametaka waelimishwe kuhusu hasara za matumizi ya mkaa na athari zake kimazingira. Nishati jadidifu ni pamoja na umeme jua, upepo na umeme wa maji,

Mkufunzi wa Jeografia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Godwin Lema, alishauri wakati akizungumza kwenye mdahalo uliohusu nishati jadilifu ulioandaliwa na shirikla lisilo la kiserikali la Human Dignity and Environmental (Hudeko) na kushirikisha wanafunzi, viongozi na wadau wa nishati nchini.

Pamoja na mambo mengine mdahalo huo, ulijadili kuhusu ukinzani unaokwamisha jamii kwenye matumizi ya nishati jadilifu, na iwapo serikali na taasisi zinafanya jitihada kufanukisha nishati hiyo.

"Jamii bado inahitaji kupatiwa elimu kuhusu matumizi ya nishati jadilifu kwa sababu licha ya faida za matumizi hayo bado ni asilimia moja tu ya Watanzania wanatumia na huku matumizi mengine kama mkaa yakishamiri ilihali yana athari kubwa ya uchafuzi wa mazingira," alisema Dk. Lema.

Aidha, alisema wanatoa elimu kwa wanafunzi vyuoni kuhusu matumizi sahihi ya nishati jadilifu kwa kusaidia kutoa elimu, kufanya utafiti na kuhakikisha wanafunzi wanafuatilia maendeleo ya teknolojia.

Pia, alisema wanatoa huduma na kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kufikisha elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kutumia nishati jadilifu.

Mwanzilishi wa Hudeko, Sara Pima, alisema elimu ya matumizi ya nishati jadilifu bado inahitajika nchini na ndio sababu wamekuja na mpango wa kufanya mdahalo kila mwezi wa kujadili suala hilo.

"Tumekuja na suluhisho la mazingira kwa kutoa elimu zaidi kwa jamii. Kila mwezi tutakutana kujadili ili kuwa na uelewa mpana katika hili," alisema Pima.

Mhandisi Mkuu wa Utafiti kutoka Shirika la Umeme nchini (Tanesco), Samweli Lucas, alisema tayari wameshafanya tafiti za kutumia umeme wa nishati jadilifu katika mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, Singida, Pwani na Njombe.

Alisema katika mikoa hiyo waliangalia namna ya kutumia upepo na jua kupata umeme ili kuondokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

# Mwenyekiti wa Halmashauri kortini tuhuma uvamizi ardhi

**Na Mwandishi Wetu,**
IGUNGA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Peter Onesmo, amefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kuvamia eneo na mtu na kuliendeleza.

Onesmo na mwananchi, Ndekwanuma Buskwami, mkulima na mkazi wa Kata ya Choma wilayani humo, walipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Mwanzo ya Choma kujibu mashtaka ya kulivamia eneo la ekari mbili na kulilima.

Baada ya washitakiwa kusomewa mashitaka yao mbele ya Hakimu Saimoni Malima, Karani wa Mahakama, Jida idd, aliiomba kupangwa tarehe nyingine ya kuanza kulisikiliza shauri hilo ili kuandaa ushahidi.

Awali, washitakiwa hao wawili walidaiwa kuwa mnamo Novemba mwaka huu, walivamia shamba la Tungu Ntegu (52), mkulima na mkazi wa kata hiyo.

Washitakiwa walikana mashtaka dhidi yao na wako nje kwa dhamani wakisubiri kesi yao kutajwa tena Jumanne ya wiki ijayo.




Mjumbe wa serikali ya Mtaa wa Mikocheni Dar es Salaam, Amani Mero, akizungumza na waandishi wa habari jana, akitoa maelezo kuhusu kuvamiwa eneo la wazi na mtu asiyejulikana na kuanza ujenzi. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Mafanikio 11 Hospitali Rufani Mbeya miaka minne ya JPM

**INATOKA UK. 5**

Mkurugenzi huyo pia alisema wamefanikiwa kupunguza gharama za ununuzi wa maji tiba nje ya nchi na wana uhakika na upatikanaji wake, wametoa mafunzo ya utaalamu wa utengenezaji wa maji tiba na kuongeza ajira kwa wataalamu wa kutengeneza dawa hiyo.

"Ni matarajio yetu kuwa, mara baada ya kukidhi mahitaji ya ndani, tutaanza kuzalisha maji tiba ambayo yatauzwa katika hospitali zilizoko Nyanda za Juu Kusini na pia muda mfupi tutaanza kutengeneza dawa za macho, mchakato umeshaanza," alibainisha.

Alisema wanatarajia kuanza kutengeneza dawa ya macho na masikio kwenye kiwanda hicho mwakani.

Dk. Mbwanji alisema hospitali hiyo inahudumia mikoa saba ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Iringa, Njombe, Ruvuma, Katavi Rukwa, Songwe na Mbeya na imeendelea kuboresha huduma zake mbalimbali ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni ongezeko la upatikanaji dawa kutoka asilimia 70 hadi 95, madaktari bingwa kutoka 36 hadi 53 na huduma za kibingwa za masikio, koo na pua.

Alisema mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa kitivo cha udaktari cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Mbeya) ambako kumetoa fursa kwa madaktari kuanza kufanya utafiti, kuanzishwa kwa huduma ya mkalimani wa lugha ya alama pamoja na uwezo wa kulaza wagonjwa kutoka vitanda 477 hadi 553 baada ya kukamilika jengo la watoto.

Vilevile, alisema serikali ilitoa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Radiologia ambalo baada ya kukamilika, limefanikisha utoaji wa huduma za mionzi na kuanzisha huduma mpya za CT Scan, mashine za kidigitali za X Ray, Fluoroscopy, Mammography na Ultrasound.

Mkurugenzi huyo alisema mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa kituo cha Methadone cha kutoa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya ambacho kwa sasa kinahudumia waraibu 261.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Afya, Gerald Chami, alisema kampeni hiyo itafanyika katika kanda tano nchini kwa taasisi ambazo chini ya wizara ili kuwaeleza wananchi mafanikio ya miaka minne kwenye sekta hiyo ambayo yamesaidia wananchi kupata huduma bora za afya.

## Mbowe aanika sababu za Mnyika kumrithi Mashinji

**INATOKA UK. 2**

atakuwa Katibu Mkuu wa tano kuongoza chama hicho tangu kianzishwe rasmi Mei 1992, akitanguliwa na Bob Makani, Amani Kabourou, Dk. Wilbroad Slaa na Dk. Mashinji.

Kuhusu uongozi wa chama na uongozi wa jimbo, Mnyika alisema si kazi rahisi kuongoza chama na jimbo kwa pamoja na kwa sababu ya kile alichokiita ukombozi wa taifa, yuko tayari kuweka rehani ubunge wake.

**KAULI YA MASHINJI**

Katibu Mkuu anayemaliza muda wake, Dk. Mashinji, mbali na kukishukuru chama kwa kumwamini katika nafasi hiyo, alieleza mambo magumu aliyokutana nayo katika uongozi wake.

Aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na maandalizi ya maandamano ya kupinga kile walichokiita udikteta, maarufu Ukuta, akieleza kuwa alishangazwa na maandalizi makubwa ya vyombo vya dola nchi nzima dhidi ya maandamano hayo.

"Tulipotangaza tu Ukuta, serikali yote iliamka, majeshi yote yalikaa barabarani, ikawa ngumu kwetu kuishauri Kamati Kuu ni hatua gani za kuchukua, lakini tunamshukuru Mungu tulivuka salama," Dk. Mashinji alisema.

Aliongeza kuwa tukio la kupigwa risasi mjini Dodoma kwa Mwanasheria Mkuu wa chama hicho, Tundu Lissu, lilimpa wakati mgumu kama Katibu Mkuu wa chama kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya kitendo hicho na msukumo uliokuwapo kwa viongozi na wanachama wa chama hicho.

Jambo lingine alilodai lilimpa wakati mgumu ni hamahama ya madiwani na wabunge wa chama hicho, akieleza kuwa ingawa ilikuwa ni haki yao ya kikatiba, lakini aliona ulikuwa ni mtego wa kisiasa.

Dk. Mashinji alisema taarifa za kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu wa Chadema zilimshtua hata mke wake kwa kuwa hakuwahi kufanya siasa na hivyo alidhani kuwa ulikuwa ni utani tu wa Mwenyekiti (Mbowe), lakini baadaye aliamini kiongozi huyo wa upinzani hakuwa anatania.

Dk. Mashinji alijiunga na Chadema mwaka 2014 na kabla ya kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho mwaka 2016, hakuwahi kushika cheo chochote cha kisiasa.






Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Civil Social Protection Foundation (CSP), Nemence Iriya, akizungumzia mikakati mbalimbali ya shirika hilo juzi, kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Babati , Elizabeth Kitundu. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanasiasa wafundwa kuhusu maendeleo

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

WANASIASA wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kutowakatisha tamaa wadau wa maendeleo pindi wanaposaidia miradi ya kijamii ili wananchi wanufaike nayo.

Mwenyekiti wa Shirika lisilo la kiserikali la ECLAT Foundation, Peter Toima, alisema hayo juzi wilayani hapa wakati akitoa ahadi ya kununua mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Tanzanite iliyoko katika mji mdogo wa Mirerani.

Toima alisema wanasiasa wanapaswa kushindana kwenye maendeleo na si kunung'unika au kugawa watu baada ya kuona wengine wanapambana katika maendeleo.

Alisema kupitia shirika hilo, wametumia Sh. bilioni saba katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwa jamii, hivyo wanasiasa wengine waige maendeleo badala ya kupigana vita.

"Tunagombana kwa sababu gani? Kama mwenzako amefanya maendeleo hapa Simanjiro na wewe fanya ili hasira imalizike na si kunung'unika kwani mimi nitafanya sana," alisema Toima.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alimshukuru Toima kwa kujitolea mifuko ya saruji akisema itasaidia ujenzi wa madarasa ya shule hiyo kukamilika kwa wakati.

"Awali ulitoa mabati 50 ya kuezekea madarasa mawili ya Shule ya Sekondari ya Benjamini William Mkapa, yaliyoezuliwa na upepo, kisha matofali 4,000 ya Sekondari ya Tanzanite na hii mifuko 100 ya saruji tunashukuru sana," alisema Kobelo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tanesco, Justin Sarakikya, alisema wadau wa maendeleo kama Toima ni watu wa kukumbatiwa kwa kuwa si atu wa maneno ila wanaonyesha kwa vitendo kwa kuacha alama za maendeleo katika maeneo tofauti.

"Kuna wanasiasa tuliwapa nafasi lakini hawakuacha alama yoyote hata ya kujenga choo cha shimo ila huyu Toima si kiongozi na amefanya mambo mengi ya maendeleo hapa Simanjiro bila kugawa watu," alisema Sarakikya.

Katibu wa CCM Kata ya Mirerani, Michael Mwakiboro, alimshukuru Toima kwa kujitolea kusaidia jamii, hasa ya Mirerani kwenye suala zima la maendeleo na aendelee na moyo huo.

# Wajasiriamali waelimishwa ubunifu bidhaa bora

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MIRERANI

WAJASIRIAMALI 50 wa Mji mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kubuni biashara zenye tija kwa jamii badala ya kupoteza muda kwa kuiga biashara ambazo zitawaingizia hasara.

Mtaalamu wa Saikolojia wa jijini Arusha, Joseph Mrindoko, aliyasema hayo juzi eneo la Mirerani, wakati akiwajengea uwezo wajasiriamali hao kwenye ukumbi wa Mazubu Grand uliopo mjini hapa.

Mrindoko alisema wajasiriamali wanapaswa kufanya kazi kupitia maono waliyo nayo tangu utotoni ili wapate mafanikio. "Nafahamu biashara nzuri ile yenye mvuto katika jamii uliyopo na uliyobuni mwenyewe si kuiga mwenzako. Mkibuni biashara zilizo katika ndoto zenu, mtafika nazo mbali maana zitakuwa endelevu na si mfu," alisema.

Kwa mujibu wa Mrindoko, kanuni za maisha zinaeleza usipofanya chochote hautapata chochote na kadiri unavyofanya ndiyo utakavyopata, hivyo wasibweteke kwenye maisha yao.

"Akili ya binadamu ina sehemu tatu tuzitumie zote na ukiwa duniani. hakikisha unaacha alama tusilale mchana. Mfano mimi huu mwaka wangu wa nane nalala kwa muda wa saa nne pekee kwa siku na wala sijaugua ugonjwa wowote," alisema Mrindoko.

Mmoja wa wakurugenzi wa asasi ya Tanzanite Mining Tourism, Charles Mnyalu, alisema kupitia mafunzo hayo wajasiriamali hao wataongeza uelewa na kunufaika wenyewe na jamii zao.

Mnyalu alisema Tanzanite Mining Tourism wamedhamini mafunzo hayo kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuwanyanyua kiuchumi wajasiriamali hao kupitia elimu hiyo.

Mkurugenzi mwenza wa asasi hiyo, Nuru Mkirery, alisema mafunzo hayo yametolewa bila malipo kwa lengo la kuwajali wajasiriamali hao ili wachangamkie fursa mbalimbali zilizopo.

"Mwalimu Mrindoko amewafundisha wajasiriamali hawa watoke kwenye duara walilopo na kufikiria nje ya hapo kwani binadamu akitumia akili aliyonayo ambayo ni rasilimali aliyo nayo, anaweza kunufaika maishani mwake," alisema Mkirery. Mmoja wa wajasiriamali walioshiriki mafunzo hayo, Hamis Seif, alisema anatengeneza na kuuza mabegi na amefaidika kwa elimu hiyo ikiwamo kuwekeza kwenye muda.

"Katika mafunzo haya nimejifunza pia umuhimu wa kuwa mtanashati kwani mara nyingi watu wanakihukumu kitabu kutokana na mwonekano wa jalada lake na si kurasa zilizo ndani yake, hivyo tunapaswa kubadilika," alisema.

# Mbunge avisaidia vikundi vya wajane

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MBUNGE wa Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo, ametoa msaada wa Sh. milioni moja kwa vikundi vya wajane na watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwenye Kitongoji cha Makisoru Kijiji cha Nguruma wilayani humo.

Akizungumza jana wakati akikabidhi msaada huo, Dk. Pallangyo alisema ametoa fedha hizo ili kuongeza nguvu katika mitaji yao ya kuweka na kukopa, kwenye vikundi vya Fanikiwa na Upendo.

"Naamini mtakuza mitaji yenu kwenye ujasiriamali mnaoufanya na kuinuka kiuchumi tofauti na sasa. Kikubwa naomba kila mmoja akope kwa malengo na si kufuata mkumbo ili mwisho wa siku kila mmoja aongeze uzalishaji katika shughuli anayofanya," alisema.

Pia aliahidi kutoa matofali 1,000 kusaidia ujenzi wa Shule ya Awali ya Elishadai, inayosaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, kutoka kaya zenye kipato cha chini ili wapate elimu bora.

Aidha, alisema serikali itaendelea kuunga mkono vikundi vya kinamama kwa kuhakikisha halmashauri zote nchini zinatekeleza agizo la kukopesha vikundi hivyo asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Arumeru, Hungura Mbwana, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa mbunge na serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Msimamizi wa vikundi vya wanawake wajasiriamali, Regista Fredy, alisema vikundi hivyo vinafanya shughuli mbalimbali ikiwamo ufugaji wa mbuzi wa maziwa ambao watagawiwa na mbunge huyo kwa wale ambao hawakupata ili kujikwamua kiuchumi.

Mwanzilishi wa Shule ya Elishadai, Fred Kulungwa, alimshukuru mbunge huyo kwa kuwapatia matofali yatakayosaidia kukamilisha ujenzi wa shule hiyo yenye uhitaji mkubwa katika kitongoji hicho.

# Waliohujumu mradi watakiwa 'kutubu'

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WATU wanaodaiwa kuhujumu mradi wa umwagiliaji wa Kalimawe wilayani Same ambao wamo viongozi wa serikali, wamepewa nafasi nyingine ya kutubu hadharani na kisha kuirejesha mitambo ya kufua umeme wa jua iliyochukuliwa kiutata.

Wanaotuhumiwa wanadaiwa kuing'oa mitambo huyo na kuiondoa eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe jana kuhusiana na hujuma hiyo.

Watu wanaodaiwa kuwa viongozi wa umma wakishirikiana na baadhi ya wananchi katika Kijiji cha Karamba, Kata ya Kalimawe, waling'oa mitambo hiyo iliyokuwa ikitumika kusukuma maji.

"Nyie viongozi wa Karamba na wengine mnaojua mmeshiriki kuukwamisha mradi huu wa umwagiliaji, rejesheni solar zilizokuwa zinatumika kusukuma mitambo ya maji. Baada ya siku 30 kupita, nitalia na nyie.

"Suala la kurejesha 'solar' hizo ni agizo la Waziri, naomba sana msimchonganishe waziri, serikali na wananchi wake."

Mkuu huyo wa wilaya aliwataka wakazi Karamba kuheshimu na kuendelea kushirikiana na vijiji vingine vinavyolizunguka Bwawa la Kalimawe vinavyotekeleza mradi wa kuzalisha vifaranga vya samaki.

Mwaka jana, vijiji vinne viliingia makubaliano ya ubia katika uwekezaji huo na kampuni ya Norway na ile ya Mikono Tayari ya Tanzania.

Kampuni hizo zimeahidi kujenga kiwanda cha kisasa cha kusindika minofu ya samaki kwa ajili ya soko la ndani na la kimataifa.

Bwawa hilo lenye urefu wa mita 4,000 na upana wa mita 5,000 lilijengwa na serikali ya wakoloni, kati ya mwaka 1952 na 1959.

# DC ataka changamoto kuwa fursa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imesema suala la ukuaji wa mji wa Moshi haliepukiki, huku ikitaka changamoto zote zinazotokana na mchakato huo zitumike kama fursa katika mpango kabambe unaondaliwa hivi sasa ambao utakuwa dira na mwelekeo wa miaka 20 ijayo.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akifungua kikao kazi cha kujadili mpango kabambe wa mwaka 2019/2039 kuhusu mchakato wa uandaaji wa upanuzi wa mji wa Moshi.

"Ndugu zangu suala la ukuaji wa mji huwa haliepukiki, hivyo changamoto zote zinazotokana na ukuaji wa mji zitumike kama fursa na kuhakikisha zinawekwa katika mpango kabambe. Naomba sana mzingatie mahitaji ya wananchi mnapojadili ili mpango huu uwarahisishie wananchi katika shughuli zao maendeleo," alisema. Manispaa ya Moshi ilikaa na wadau mbalimbali kujadili mpango huo wa upanuzi wa mji wa Moshi utakaotekelezwa kati ya mwaka 2019/2039.

Alisema suala kubwa katika mpango kabambe huo ni kujua shughuli zote za kijamii, kiuchumi, kiutawala na kimazingira zitakazofanyika juu ya ardhi. "Ni muhimu kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kutumia rasilimali hiyo kwa ufanisi na kuleta maendeleo endelevu. Ni matumaini yangu kuwa mpango huu utakapokamilika tutahakikisha kuwa tunautekeleza ili uweze kusimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo na ukuaji wa Manispaa yetu," alisisitiza.

Aprili, mwaka jana, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Dk. Anna Mghwira, alinukuliwa akisema serikali imetoa masharti mawili yanayopaswa kuzingatiwa na Manispaa ya Moshi ili kulipatia ufumbuzi pingamizi lililowasilishwa kwa Rais John Magufuli kuhusu mchakato wa upanuzi wa mji wa Moshi unaotaka kupewa hadhi ya kuwa Jiji.

Mkuu huyo wa mkoa alisema tayari ameshapokea maelekezo ya nini kifanyike katika kutekeleza maelekezo ya Rais Magufuli ambayo ni kuendelea kuandaliwa mpango kabambe utakaoshirikisha halmashauri zote tatu za Hai, Moshi na Manispaa ya Moshi. Baada ya mpango kuandaliwa kila halmashauri itasimamia maendeleo kwenye eneo lake. Iwapo Rais Magufuli ataweka baraka zake, mpango huo utamega kilomita za mraba 16 za Wilaya ya Hai na kilomita 68 za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kuifanya Manispaa ya Moshi kuwa na kilomita za mraba 142.

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa sasa iko katika mpango maalum wa utayarishaji wa mpango kabambe wa mwaka 2017/2039 utakaoiwezesha kuwa Jiji.

Kazi hiyo ya utayarishaji wa mpango kabambe inafanywa na mtaalam mshauri M/S CRM Land Consult (T) ambaye anashirikiana na City Plan Consultants Ltd, Norplan (T) Ltd na Y& P (T) Architects Ltd, zote za Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Lengast, Kata ya Naisinyai, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Tulipo Mamasita, akizungumzia mikakati na changamoto kwenye mkutano wa kijiji hicho juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mikopo makundi maalum kukuza uchumi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

HALMASHAURI ya Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro imesema mkakati wa serikali wa kuhimiza kila wakati utoaji wa mikopo ya uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, unalenga kutoa fursa kwa makundi hayo kuwa na kipato halali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Anna-Claire Shija, alitoa kauli hiyo jana wakati wa hafla ya kukabidhi mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 110 kwa vikundi 29 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kabla ya kukabidhi mikopo hiyo, alisema uamuzi huo wa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli ina nia njema ya kutaka kuona hali ya uchumi ya kila mwananchi inaongezeka kwa wastani, wakati taifa likielekea katika uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Uamuzi wa serikali wa kuwahimiza vijana, wanawake na walemavu wajiunge kwenye vikundi ili kuweza kupatiwa mikopo ni namna ya kuwaweka pamoja watu wenye ujuzi na uzoefu tofauti. Serikali inaamini watu wote wana uwezo wa kufanya kazi za kujiingizia kipato halali na si dili wala michakato ya kifisadi," alisema Shija. Alisema fedha hizo zilipatikana kutokana na makusanyo ya mapato ya ndani kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2019/20.

Kwa munjibu wa Shija, utoaji wa mikopo hiyo ni agizo la Rais Magufuli kwamba kina mama na vijana wapewe mikopo isiyo na riba kutoka katika mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, Mkurugenzi huyo aliwahakikishia wakazi wa Same kwamba halmashauri hiyo itaendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya kinamama na vijana na kuwataka walengwa hao waunge mkono juhudi hizo kwa kufanya kazi kwa bidii, kulinda mapato ya halmashauri yasipotee na kurejesha kwa wakati ili zoezi liwe endelevu.

Awali, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, alisema serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli imeondoa riba kwa vikundi vyote vinapochukua mkopo ili kuwaondolea umasikini Watanzania hasa wanawake, vijana na walemavu.

"Mikopo hii ya asilimia tano inayotolewa kwa wanawake na vijana na walemavu inatokana na makusanyo ya ndani kwa ajili ya kuliwezesha kila kundi. Ni sera ya serikali lakini kuna changamoto zake ambazo tunaziona, moja ikiwa kutorejeshwa kwa wakati fedha hizi ili ziwanufaishe na wengine. Pia baadhi yao hasa vijana hawarejeshi," alisema.






Mfanyabiashara wa soko kuu la majengo Jiji la Dodoma, Mzee Langolango, akipanga embe kwa ajili ya kuuza kwa wateja wake **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Walalamikia kukopwa milioni 200/- za zabibu

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAKULIMA wa zabibu wa Kijiji cha Mvumi Muungano wilayani Chamwino, wameandamana hadi kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kulalamikia kucheleweshewa malipo yao.

Wakiwa katika ofisi ya Dk. Binilith Mahenge, walieleza kuwa wanadai Sh. milioni 200, kutoka kampuni ya usindikaji wa mvinyo ya Dane Holdings Limited ya Nkulabi jijini hapa.

Wakulima hao wakizungumza na wanahabari nje ya jengo la ofisi ya Mkuu wa Mkoa walisema kuwa ni zaidi ya miezi minne sasa tangu wafanye biashara na kampuni hiyo lakini mpaka sasa bado hawajalipwa fedha zao.

Mmoja wa wakulima hao Veronica Mkunda, alisema kuwa waliiuzia kampuni hiyo zabibu tangu Agosti mwaka huu lakini wamekuwa wakizungushwa kupata malipo yao jambo ambalo linawafanya kuwa na maisha magumu kila kukicha.

"Sisi ni wakulima na tumeiuzia kampuni zabibu ili kujikimu lakini cha kushangaza hatujalipwa kwa wakati,"alisema na kuongeza: "Kutokana na hali hiyo aisha yetu yamekuwa mabaya kwani tunashindwa hata kuandaa mashamba, tunakwama kulipa ada za watoto wa shule, hatujui tutafanyaje, lakini pia huu ni msimu wa sikukuu tutawezaje kusherehekea?"

Alisema kutokana na hali hiyo wanaiomba serikali kuingilia kati suala hilo ili walipwe fedha zao na waendele na shughuli nyingine za kuandaa mashamba kwajili ya msimu wa kilimo. Aidha, waliiomba serikali ili kuondokana na adha hiyo wakati mwingine iwatafutie masoko ya uhakika ili wauze mazao yao na kupata fedha kwa wakati.

"Tumekuwa tujikuta tukikopesha kampuni zabibu zetu na wakati huohuo tunatumia gharama kubwa kuandaa mashamba jambo ambalo linakatisha tamaa,"alisema.

Aidha wakulima hao walisema licha ya kuwa kilimo cha zabibu kuwa cha gharama kubwa lakini hawanufaiki nacho kutokana na kukosa soko la uhakika.

Alisema kutokana na kukosekana kwa soko la uhakika wanunuzi wamekuwa wakijipangia bei wanayoitaka jambo ambalo linamfanya mkulima kuendelea kuwa masikini.

Akijibu malalamiko hayo Mkurugenzi wa Dane Holdings Limited, Danford Semwenda, alisema kuwa ni kweli wakulima hao wanadai zaidi ya Sh. milioni 200. Hata hivyo, Semwenda alisema kuwa ifikapo Januari 8, mwakani wakulima hao watakuwa wamelipwa fedha zao zote kwani hata yeye kuna kiasi cha fedha anadai bado hajalipwa na wadeni wake.

## Ndejemba ataka wazazi,walezi kuchangia ujenzi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, ametaka wazazi na wazazi kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kuchangia elimu ili watoto wapate elimu bora itakayowawezesha kutimiza ndoto zao.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akipokea msaada wa vifaa mbalimbali vya elimu ikiwa ni mchango wa benki ya NMB, vilivyokabidhiwa katika Mji mdogo wa Kibaigwa Wilayani Kongwa.

Ndejembi, aliwataka wazazi kuunga mkono juhudi hizo kwa kuchangia ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya elimu.

"Ndugu zangu tukitaka kufikia malengo ya elimu ni lazima tuwe pamoja msisubiri wahisani peke yao kutusaidia, kwanza ni sisi wenyewe tuonyeshe mfano wazazi na walezi ili watoto hawa wafikie ndoto za kupata elimu,"alisema.

Aliwaambia wananchi wakionyesha juhudi zao katika ujenzi wa miundombinu ndipo wadau wengine watawaunga mkono kumalizia baadhi ya miradi itakayoonekana kukwama.

Aidha, alisema Wilaya ya Kongwa inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 39, kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wa kidato wa kwanza mwaka 2020.

Alibanisha kuwa wanaendelea na kuwahamasisha wananchi katika maeneo mbalimbali kuchangia ujenzi wa vyumba hivyo ili wanafunzi hao waanze masomo mapema mwakani.

Pia aliwaomba wadau wengine wa elimu kujitokeza kuchangia katika halmashauri hiyo ili kufikia malengo ya utoaji wa elimu bora.

Ndejembi aliishukuru Benki ya NMB kwa kuwapatia msaada wa vifaa hivyo vya elimu katika Wilaya hiyo kwani vimepunguza changamoto.

Kwa upande wake Meneja wa NMB Kanda ya Kati Nsolo Mlozi, alisema taasisi hiyo imekabidhi msaada wa vifaa vya madawati, viti na meza pamoja na mabati ya kuezekea vyumba vya madarasa vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 25.

Mlozi alizitaja shule zilizopokea vifaa hivyo kuwa ni Machenje, Masenha, Muungano na Miembeni ambazo zote zilipokea msaada wa mabati kwa ajili ya kuezekea vyumba vya madarasa vikiwa na thamani ya Sh. milioni 15.

Nyingine zilizonufaika na msaada huo kuwa ni shule za Sekondari Kibaigwa na Kinangali ambazo zimepatiwa meza 100 na viti vyake vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 10.

## Tanroads yatumia bilioni 16/- kujenga miundombinu

**Na Paul Mbaeja,** DODOMA

KAIMU Meneja wa Wakala wa Taifa wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Dodoma, Salome Kabunda, ameeleza kuwa katika bajeti ya mwaka 2019/2020 mikataba 33 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja imesainiwa na kazi zinaendelea kutekelezwa.

Aidha, Kabunda amesema mikataba hiyo ina thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 16, ambayo ni sawa na asilimia 88 ya bajeti na imesainiwa katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Novemba mwaka huu.

Aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha bodi ya barabara mkoa wa Dodoma, kilichofanyika jijini hapa.

Pia, alisema kuwa katika mwaka wa fedha wa 2019/20, Tanroads imeidhinishiwa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 1,138 pamoja na madaraja 352.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya barabara inayosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura), katika kikao hicho cha bodi ya barabara , Mratibu wa Wakala Mkoa wa Dodoma, Lusako Kilembe, alisema wanahudumia kilomita 6,996.25 ambapo mpaka sasa wameshapokea Sh. bilioni 2.456 sawa na asilimia 17.


Alisema pamoja na kupokea kiasi hicho cha fedha lakini bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo matumizi mabaya ya mabarabara. "Lakini pia kuharibika kwa barabara kutokana na mvua zinazonyesha hivi sasa kama ambavyo imesemwa hapo awali kule wilayani Kondoa lakini pia makandarasi kutokuwa waadirifu ambao tumekuwa tukiwapiga tozo mbalimbali kutoka na kuchelewesha miradi,"alisema

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Binilith Mahenge, akifungua kikao hicho aliwataka wajumbe wa bodi ya barabara kuhakikisha wanatoa mawazo yao yatakayosaidia kuweka mipango thabiti ya kurudisha miundombinu ya barabara iliyoharibika kutokana na mvua.

Akifungua kikao hicho jijini hapa Dk. Mahenge alisema anajua kipindi hiki cha mvua kuna baadhi ya miundombinu ya barabara imeharibika hivyo ni vyema fedha za Watanzania kutumika vizuri katika kurudisha miundombinu hiyo kama ilivyokuwa awali.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya Sh. bilioni 10.9 zimeidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendelo ya barabara zenye urefu wa kilomita 84 katika Mkoa wa Dodoma kupitia bajeti ya maendeleo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, aliipongeza serikali kwa kutelekeleza Ilani ya chama hicho kwa vitendo katika sekta ya miundombinu ya barabara.





Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na wanafunzi wa Madrasa ya Qurian ya Mpitile iliopo katika Kijiji cha Moga, Wilaya ya Kaskazini (A), Mkoa wa Kaskazini Unguja wakati alipotembelea kijiji hicho. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Amuua mke wake kwa kisu naye kujinyonga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTU aliyefahamika kwa jina la Khamis Nassor (39) mkazi wa Mwera, Unguja, anadaiwa kumuua mkewe kwa kumchoma kisu kisha kujiua kwa kujinyonga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharini, Awadh Juma, alisema tukio hilo lilitokea juzi likihusishwa na wivu wa kimapenzi.

Kamanda Awadh alisema Nassor ambaye sasa ni marehemu, kabla ya kujiua, alitenda kosa la kumuua mkewe, Mariam Thomas Zakaria (35) baada ya kuwapo kwa tuhuma za wivu wa mapenzi kati yao.

Alisema Nassor alikuwa akimtuhumu mkewe kuwa na uhusiano na watu wengine na ndipo alipochukua sheria mikononi kwa kumchoma kisu mkewe hadi kusababisha kifo.

"Jeshi la Polisi linafanya uchunguzi zaidi kuhusu tukio hili la mauaji ya Mariam aliyeuawa kikatili na mumewe kwa kumchoma kisu,' alisema. Kamanda Awadh alisema wakati wakifanya juhudi za kumtafuta mhusika wa tukio la mauaji, walipata taarifa kwamba kuna mtu amejinyonga huko Mtofaani Mwera na walipofanya uchunguzi zaidi walibaini kuwa ni mtu aliyehusika na mauaji ya mkewe.

"Tunaendelea kufanya uchunguzi zaidi kuhusiana na tukio hilo. Tulikuwa tukimtafuta mwanamume aliyesababisha mauaji kumbe na yeye amejinyonga," alisema Kamanda Awadh.

Tukio hilo ni la pili kutokea kwa wanawake kuuawa kwa kuchomwa kisu na waume zao kwa mwaka huu Zanzibar kisha waume hao nao kujiua kwa kujingonga.

# Mvua zakwamisha ujenzi barabara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MVUA za vuli zinazoendelea kunyesha visiwani Zanzibar, zimeelezewa kuwa ndizo zinazokwamisha kazi ya kutandika lami kwenye barabara itokayo Koani hadi Jumbi Wilaya ya Kati Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mhandisi Mkuu wa Kampuni ya Ujenzi ya MECCO, Nassor Ramadhan Kolowa, alisema kazi hiyo ilikwishaanza na kufikia hatua ya kuweka lami nyepesi upande wa Jumbi kwa kilomita nne.

Hata hivyo, alisema katika kujenga barabara, kunajitokeza changamoto mbalimbali ambazo zingine zinakuwa nje ya uwezo wa mwanadamu, hivyo wanapambana ili kuhakikisha wanamaliza kazi hiyo kwa muda uliopangwa, mwishoni mwa Februari, mwakani.

"Neema ya mvua ni kudra ya Mwenyezi Mungu na inaponyesha huwezi kumwaga lami kwa ajili ya kujenga barabara. Kama si mvua hii inayoendelea, kazi hii ingekuwa imefika mbali au karibu kukamilika," alisema Kolowa.

Alisema kutandika lami wakati mvua inaponyesha si jambo la kitaalamu na kufanya hivyo ni kutafuta hasara ambayo ikitokea haiwezi kufidiwa kwa kuwa itakuwa kinyume cha maelekezo.

Pamoja na changamoto hiyo, Mhandisi huyo alieleza matumaini yake kwamba ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 6.03 utamalizika ndani ya wakati uliopangwa mwishoni mwa Februari.

Baadhi ya wakaazi wa Koani, walisifu kazi nzuri inayofanywa na MECCO huku wakiomba kuwekewa kifusi kingi zaidi kwenye njia mbadala inayopita kando ya nyumba zao.

# SMZ: China inayatambua Mapinduzi ya Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema China ni miongoni mwa nchi za mwanzo duniani kuyatambua Mapinduzi ya Zanzibar, hivyo kusaidia harakati za kujenga uchumi na kuleta maendeleo Zanzibar.

Pia imesema katika kipindi cha miaka tisa kuanzia mwaka 2000, Zanzibar imefaidika na misaada mikubwa iliyotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China yenye thamani ya Sh. Bilioni 306 na kusaidia katika kuleta maendeleo na kukuza uchumi na ustawi wa wananchi wake.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, wakati akizungumza katika mkutano uliowakutanisha wanafunzi waliosoma China katika ngazi mbalimbali. Alisema nchi hiyo ilisaidia kwa kiasi kikubwa ujenzi wa maendeleo ikiwamo sekta ya elimu na ujenzi wa miradi ya viwanda mbalimbali vikiwamo vya kati.

Balozi Ramia alisema baadhi ya viwanda vilivyojengwa na nchi hiyo ni kilichokuwa kiwanda cha ngozi na viatu, sigara, matrekta kilichoko Mbweni pamoja na kujenga uwanja wa michezo wa Amaan ulioko Unguja.

"China mara baada ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 walitusaidia katika juhudi za kulijenga upya taifa la Zanzibar, hivyo kusaidia miradi ya ujenzi wa viwanda mbalimbali," alisema.

Pia alisema nchi hiyo tangu mwaka 1965 hadi sasa, imeleta madaktari awamu ya 29 na kufikia timu ya madaktari 740 waliotoa huduma za matibabu Zanzibar.

"China wamekuwa wakitusaidia katika sekta ya afya kwa kuleta madaktari bingwa tangu mwaka 1965 na sasa sasa wameifanyia ukarabati mkubwa hospitali ya Abdalla Mzee iliyoko Pemba,' alisema.

Aliutaja msaada uliotolewa hivi karibuni na China wa Sh. bilioni 33 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za madaktari na wafanyakazi katika hospitali ya Abdalla Mzee.

Akizungumza katika sherehe hizo za kuwapongeza wafanyakazi waliopata mafunzo mafupi nchini China, Balozi Mdogo wa China nchini, Xie Xiaowu, alisema tayari nchi hiyo katika kipindi cha miaka minne imetoa nafasi 126 za masomo kwa wanafunzi wa ngazi ya shahada ya kwanza.

Balozi huyo pia alisema katika kipindi cha miaka minne, wanafunzi 700 wamepata nafasi za mafunzo ya muda mfupi nchini China. "Kwa ufupi idadi ya watu waliopata mafunzo mbalimbali ya ufundi ya kitaalamu kutoka China imeongezeka na kufikia 380," alisema.

Jamhuri ya Watu wa China iliyatambua Mapinduzi ya Zanzibar na kufungua ubalozi mdogo ambao umedumu hadi sasa ukiwa na lengo la kufuatilia kwa karibuni misaada inayotolewa na nchi hiyo.



**OMOTOLA WEWE SIKU NYINGINE USIRUDIE**

Soma UK.20

JUMAMOSI DESEMBA 21, 2019

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



## 'LOVE STORY'

# Wakenya wajiuliza, Tanzania wagunaguna

BASI SAWA

# NILLAN Zao la Burudani anayetoa onyo kwa wakongwe

MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi katika muziki wa Bongofleva, Nillan, ametambulisha kibao chake kipya kinachoitwa 'Zombo' na kujinasibu kwamba wimbo huo ni zao la muziki mpya Tanzania.

Akizungumza na BT, Nillan ambaye singo yake ya kwanza 'Njenje' omefanya vizuri, amesema wimbo wake huo mpya umerekodiwa na studio ya Free Nation na video yake imetengenezwa na Wanene.

Amsema kutoka kwa wimbo huo ni juhudi zinazofanywa na uongozi wake mpya chini ya Mhini na Mboke ambao ni wamiliki wa shule ya sekondari inayokuza vipaji ya East Coast ya mjini Kibaha.

"Nafurahi kutambulisha wimbo wangu na manejimenti yangu mpya ambayo imefanya juhudi kubwa kuhakikisha narudi katika muziki kwa kasi na ladha mpya katika muziki wa Bongo fleva," amesema Nillan.

Nillan ameongeza kwamba baada ya kuachia ngoma hiyo, kuna zingine nane zinakuja hivi karibuni na akawataka mashabiki waike kumuunga mkono kwa kuzipokea vizuri.

"Nawaomba mashabiki wangu waanze kupokea nyimbo zangu zote, bila wao siwezi kuwa Nillan kama nilivyo nahitaji nguvu zao," amesisitiza.






# Tamasha Siku ya Wasafiri laandaliwa

MSANII mkongwe wa muziki wa kizazi kipya Raymond Bruno, maarufu kama K-Zi, ameamua kuanzisha tamasha la kipekee la burudani litakalowahusisha watu wanaosafiri kutoka nchi moja hadi nyingine.

Akizungumza na BT hivi karibuni, Bruno amesema tamasha hilo litafanyika kila Oktoba 17 kila mwaka ambayo ni maalumu kama siku ya wasafiri Duniani.


Amsema tamasha hilo ambalo ni geni kwa Watanzania kutatolewa umuhimu wa watu kusafiri pamoja na kutumia kadi za posta kwa ajili ya kukumbukana.

Bruno ambaye ni mbunifu wa kadi hizo amesema jamii itapata ujumbe na kujifunza mengi kupitia kadi za aina hizo ambazo katika mataifa mengine imekuwa jambo la kawaida katika maisha ya kila siku.

"Wakati wa tamasha tutatoa kadi bure kwa watakaohudhuria ili kuwapa uzoefu, Watanzania hatupo kisiwani lazima tujifunze kwa wenzetu na nimeamua kuleta utaratibu huu hapa kwetu," amesema Bruno.

## INSTA-TWITTER





**Wanaume** wote wenye vitambi, tafadhali leteni CV zenu. Kuna watu wanatafuta 'Father Christmas'-**Ray C.**



**Mwenye** roho nzuri ana roho mbaya pia. Huwezi tu kuiona, kaificha kwenye box la hasira zake-**Mr Blue.**



# hantom Musica atambulisha ibabe 'Sitobadilika'

**Moshi Lusonzo**

DI la muziki wa dansi chini ya utaratibu wa 'Zing g' , Phantom Musica International, limekamilisha kodi wimbo mpya unaojulikana kwa jina la 'Sito-lika'.
kurugenzi Mtendaji wa kundi hilo, Abdulfareed sein ambaye ndiye mtuzi wa wimbo huo, amesema a, kibao hicho kimerikodiwa kwa kuwashirikisha dhi ya wanamuziki mahiri ambao waliimba nyimbo za nyuma.
dulfareed aliwataja wanamuziki hao ni, Juma ere, Edo Sanga, Fadhili Musafi na Tatien Budas, rufu kama 'King Budas' .
awa ndiyo walionogesha katika idara ya sauti wak-ozwa na Juma Kakere anayetajwa kuwa na sifa wa ya kupangilia sauti kwa ustadi mkubwa" alisema ed.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...



# 'LOVE STORY'

# Wakenya wajiuliza, Tanzania wagunaguna

WAKATI mwanamuziki wa Bongo Fleva, Ali Salehe Kiba maarufu 'Alikiba' amefunguka kwa kumkana mrembo wa Kenya ambaye alidai walikuwa kwenye husiano wa kimapenzi, maswali mengi yameibuka ambayo yanahitaji majibu ya kina.

Mwanadada huyo ambaye pia ni muigizaji akitokea Kenya, Bridget Achieng, aliiambia radio Jambo ya nchini humo kwamba aliwahi kuwa na husiano huo na Kiba kwa muda mrefu na kisha waliachana.

Bridget amesema katika mahojiano hayo waliachana na msanii huyo baada ya kushindwa kwenda sawa kwani yeye ana mambo ya haraka zaidi na Alikiba ni mtaratibu sana na mswahili.

Akijibu madai hayo, Kiba alimkana kwamba hamfahamu na yeye anamchukulia kama shabiki tu. Hata hivyo katika mitandao ya kijamii baadhi ya mashabiki wake wameibuka na hoja nyingi ambazo majibu yake yanahitaji kuwapo na tafakari na usahihi wa hali ya juu.

Kwanza watu hao wanahoji kwa nini Bridget amtaje yeye Kiba wakati Tanzania kuna wanamuziki wengine wenye mafanikio? Lazima kuna jambo linafichwa na kunahitaji majibu ya kina.

Pili Tatoo ambayo mrembo huyo ameonesha imeonekana kuchorwa kwa muda mrefu, kuna ushahidi kificho kuwa pengine wawili hao kuna mambo mengi wanayafahamu na hawataki kuyaibua.

Tatu, pengine jambo hilo linaweza kuwa kweli lakini Kiba kutokana na tabia yake ya usiri hataki kuwa wazi kwa kuhofia kumharibia. Lakini jambo hilo lilitokea zamani kwani kuna ubaya gani akawa muungwana kukiri ili suala hilo limalizike haraka?

Majibu ya maswali hayo ya mashabiki Kiba mwenyewe na pengine Bridget anaweza kusaidia kutoa ufafanuzi wa kina.

# Harmonize anapozungumzwa vibaya King Music

MSANII wa muziki kutoka lebo ya King's Music, Abdu Kiba amesema Harmonize si tishio kwa kaka yake kwa sababu hamfikii kwa kila kitu.

Akizungumza na Ayo Tv, Abdul Kiba, amesema mwanamuziki huyo hata yeye mwenyewe hawezi kufananishwa naye na wanaofanya hivyo watakuwa wanakosea.

"Huwezi kumzungumzia Harmonize ukamuweka Ali labda ungefikiria kwa kina Chidy, Killy au Kituga kwa sababu hata bado kwa Young king hajafika, sitaki kuzungumzia sana lakini huwezi kumfananisha na king ikiwa hata kwangu mimi hajafika," amesema Abdukiba



## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Hapa** kinachonikchekesha ni kwamba umri unavyozidi kwenda kupata picha nzuri ni kazi-**Faiza Ally.**



**Kama** huna akili usioe, maana maandiko yanasema ishini na wake zenu kwa akili-**Kala Jeremiah.**



**Pata** kidogo ushukuru, hata ukikosa usikufuru-**Billnas.**

Kuumbe!



## MUZIKI UNASIKIKA

# Wasanii wanapopambana kurekebisha jamii

MUZIKI una sikio pana na ndio maana sanaa hiyo inapendwa na watu wengi kuliko nyingine.

Wasanii wa muziki wanatajwa kama vinara wa kuielimisha, kuburudisha, kuliwaza na kukosoa jamii, asipotekelezwa hayo basi kazi yake haijakamilika.

Lakini je, wasanii wa muziki wa Afrika Mashariki wameweza kuielimisha na kuikosoa jamii?

Katika kile ambacho kilionekana kama njia ya kuikosoa na kuielimisha jamii, King Kaka kwa jina lake halisi Kennedy Ombima, mwishoni mwa juma alitoa video tata ya wimbo aliouta 'Wajinga Nyinyi', akikosoa maovu miongoni mwa Wakenya.

Katika wimbo huo amewatuhumu wazi wazi watu binafsi aliowataja majina moja kwa moja pamoja, wabunge na taasisi za umma kutokana na ufisadi na maovu mengine.

Aliutumia wimbo huo huwatolea wito Wakenya kutafakari ujumbe wa video yake na kuchukua hatua. Tangu video ya wimbo huo kutoka, imekuwa ndio maarufu zaidi mitandaoni nchini Kenya.

Licha ya wimbo 'Wajinga nyinyi' ulioimbwa kwa mtindo wa rap kusifiwa na wengi kuwa maudhui yake yalikua ni ya kweli baadhi ya waliotajwa majina walimkosoa na kutishia kumshitaki.

King kaka alidai anatishiwa maisha na kujisalimisha katika Ofisi ya Mwendesha mashitaka mkuu wa Serikali (DCI), akidai lakini ofisi hiyo ilisema haikumuita.

Mwanamuziki huyo ambaye alipata uungaji mkono mkubwa kutoka kwa wasanii wenzake kwa kutoa ujumbe huo, pia aliahidiwa utetezi wa kisheria na mawakili maarufu iwapo atapelekwa mahakamani kwa kuimba wimbo 'Wajinga nyinyi' .

Kwa muda sasa wasanii wa muziki nchini Tanzania wamekuwa wakiwasilisha ujumbe wao hususan baada ya kuingia madarakani kwa rais John Pombe Magufuli. Ukosoaji wao umekua ukijibu yanayofanyika nchini mwao.

Kalapina ambaye alishindwa katika harakati zake za kuwania ubunge, alitoa wimbo mwingine wa kumsifu rais Magufuli. Aliimba: 'Unaweza kudhani ni miujiza lakini ni picha halisi. Upinzani uko kimya, hauna la kusema. Amefanya walichopanga kukifanya.''

Nakaaya Sumari aliachia wimbo wake 'Mr politician' wa rais Jakaya Kikwete.

Ney wa Mitego alitoa wimbo, 'Wapo'. Ingawa hakutaja moja kwa moja jina lolote la kiongozi katika wimbo wake ilikua wazi kuwa alikua akielezea maeneo ambayo rais John Pombe Magufuli ' anatakiwa kutekeleza wajibu wake.

Wimbo huo ulipata umaarufu sana baada ya kukamatwa mara moja na Basata ikapiga marufuku kabisa wimbo huo.

Hata hivyo rais Magufuli aliagiza Ney aachiliwe huru na wimbo wake uchezwe. **BBC**





MIMI MARS



MAUA SAMA

# Wasanii wa kike waliotikisa 2019

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tuliwaangazia wasanii wa kiume wa muziki wa kizazi kipya, maarufu kama bongo fleva waliofanya vema mwaka 2019.

Walikuwa sita ambao ni Harmonize, Marioo, Stamina, Roma Mkatoliki, Baddest na Rayvanny.

Leo tutawaangalia wasanii wa kike ambao mwaka huu wameonekana kufanya vema. Cha kushangaza ni kwamba baadhi ya wasanii wakongwe ambao walitarajiwa kutoa ushindani mkali kama vile Mwasiti, Linnah Sanga, Ruby, hawakufanya vizuri.

Kufanya vizuri ikiwa na maana kutoa ngoma ambazo zimepokelewa vema na mashabiki wa muziki na kila unakopita, iwe kwenye mabasi, mitaani, kwenye mahoteli, migahawa, majumbani na hata kwenye sherehe mbalimbali za kijamii, hukosi kuzisikia na kuwafanya watu kupagawa kwa furaha.

Lakini hilo haliwazuii kuibuka tena na kutikisa mwaka 2020.

**VANNESA MDEE**

Katika hali ya kushangaza na isiyotarajiwa, msanii Vannesa Mdee ameendelea kuwa kwenye kiwango kile kile cha mwaka jana.

Amekuwa ni mmoja kati ya wasanii wachache wasiochuja na wanaojua kwenda na wakati.

Baada ya kufanya kutikisa sana mwaka jana, ilitegemewa labda safari hii angepoa, lakini ameendeza moto.

Ameendelea kutoa ngoma kali kama vile 'Moyo', 'Bado' ambayo amemshirikisha Rayvanny, na Never Ever'.

**MIMI MARS**

Ni mmoja wa wasanii wa kike wanaotishia umalkia wa baadhi ya mastaa wa muziki huo kwa sasa.

Mwaka huu amefanya vizuri sana na kujipatia umaarufu, hasa kwa ngoma zake kama 'Ex' remix ambao amemshirikisha Mwana FA na 'Mua'. Jumatano iliyopita ameachia ngoma yake mpya iitwayo 'Una'.





VANESSA MDEE

**NANDY**

Kuna baadhi ya watu walidhani labda ni nguvu ya soda. Ameendelea kuwaonyesha kuwa hawakuwa kweli. Ameendelea kuwa Nandy yule yule wa juzi, jana na leo.

Mwaka kwake unaisha vizuri, akiwa amewatendea haki si mashabiki wake tu, bali mashabiki wa muziki wa kizazi kipya kwa ujumla.

Ngoma zilizomuweka juu mawinguni mwaka huu ni 'Kiza Kinene' ambayo amewashirikisha vijana wa Sauti Sol, 'Hazipo', 'Magufuli Tena', na Bugana ambayo amemshirikisha msanii Billnass.

Kuna ngoma ambazo ameshirikishwa na wasanii wengine na kuzitendea haki kama 'Navimba' akishirikishwa na Sunny, pamoja na 'Haleluya' ambao ameimba pamoja na Willy Paul.

**MAUA SAMA**

Itakumbukwa kuwa mwaka jana msanii huyu alitoa ngoma moja iliyovuma kama moto nyikani, 'Iokote' ambayo pia ilimsababishia matatizo hadi kukamatwa na kulala rumande, mwaka huu haukumpita hivi hivi.

Miezi mitatu tu iliyopita, amechia ngoma kali inayotamba kwa sasa akiita 'Niteke', huku akishirikishwa na msanii G Nako kwenye ngoma moja ambayo si ya kitoto, ikiitwa 'Gusanisha'.

**ANTI VAIRAS**

Ni mwimbaji wa muziki wa uswazi, maarufu kama Singeli. Msanii huyu wa kike ameonekana kukomaa kwenye muziki huu, kwani baadhi ya waimbaji wa kike wamekuwa wakiingia na kutoka.

Yeye amekuwa na mwendelezo mzuri na mwaka huu ametoa ngoma kali akishirikisha Man Fongo iitwayo 'Cherehani'.

# Nicki Minaji akosa mamilioni kupenda vichupi

EBU fikiria unapoteza kitita kikubwa cha pesa, eti kisa, ni aina ya nguo unazopenda kuzivaa.

Ndivyo rapa maarufu wa Marekani, alipojikuta akikosa pesa baada ya kushindwa kuburudisha nchini Saudi Arabia kutokana na kupenda kuvaa vichupi  wakati anatoa burudani.

Kwanza kabla ya kuahirisha ziara hilo. Watu walishangaa baada ya kuona tangazo la kuwa Nicki Minaj atakuwa mmoja ya wasanii watakaotumbuiza katika tamasha la muziki nchini Saudi Arabia.

Tangazo hilo lilizua gumzo kali katika mitandao ya kijamii nchini humo huku baadhi ya watu wakiuliza msanii huyo atavaa nini wakati akitoa burudani?

Mtindo wake wa mavazi na maudhui ya ngono katika nyimbo zake ni baadhi ya masuala watu walihoji huku wakitafakari tamasha hilo litapokelewaje katika jamii ya kihafidhina ya Waarabu.

Rappa huyo alitarajiwa kutumbuiza watu katika tamasha la Jeddah World Fest Julai 18.

Tamasha hilo lilikuwa kama mfano wa jinsi Saudi Arabia inavyoendelea kulegeza misimamo yake mikali hasa katika masuala ya burudani ili kuimarisha ukuaji wa sekta ya sanaa.

"Nicki Minaj" alitrend katika mtandao wa Twitter baada tamasha lake la Jeddah kutangazwa.

"Hebu tafakari kupata fahamu baada ya kupoteza fahamu kwa miaka mitatu na ukizinduka kitu cha kwanza unasikia ni kuwa Nicki Minaj atafungua tamasha la muziki Saudi Arabia, kusema kweli nitafikiria niko katika taifa lingine ," mmoja aliandika ujumbe wake.

Mwingine alihoji ikiwa waandalizi wa tamasha hilo walifanya ukaguzi wa maonesho yake yaliopita japo angalau katika mtandao wa Google kabla ya kumpa kazi hiyo.

"Hivi hakuna mtu Saudi Arabia aliyemtafuta Nicki Minaj kwenye google?" aliandika mwingine kwa mshangao.

Katika video iliyowekwa kwenye Twitter mwanamke aliyevalia mavazi ya kidini alihoji kwa nini mamlaka ya nchini humo inamrusu rapa huyo kutumbuiza katika tamasha hilo huku ukiwazuia wanawake kuvaa mavazi yanayowabana hadharani.

"Atakuja kutingisha makalio yake na akiimba nyimbo zake zilizo na maudhui ya ngono huku akijitingisha zaidi," alisema  na kisha alihoji "Halafu unaniambia mimi nivae abaya. Hilo linaingia akini kweli ?"

Wengine walisema hatua ya mwanamuziki huyo kufanya tamasha nchini humo ni unafiki, ikizingatiwa kuwa anatumbuiza pia katika matamasha ya wapenzi wa jinsia moja ili hali anajua msimamo wa Saudia kuhusu uhusiano wa aina hiyo.

Minaj sio msanii wa kwanza kuzua hali ya utata kwa kukubali kufanya tamasha nchini Saudi Arabia.

Mariah Carey aliamua kufuata kitita cha pesa kwa kupuuza wito wa wanaharakati wa kutetea haki za binadamu kumuomba afutilie mbali tamasha lake nchini Saudia huku rapa Nelly nae akilaumiwa vikali kwa kuandaa tamasha la wanaume pekee.

Kutokana na maneno mshangao kutoka mitandaoni, Nicki Minaj aliamua kusema basi, alisamehe mamilioni hayo ya pesa kwa kukataa kuvaa tofauti na alivyozoea kwani yeye ni vichupi si haba.






## Sikitu Anayekumaliza wa karibu yako

**Na Adam Fungamwango**

KIKULACHO ki nguoni mwako. Ni msemo wa kiswahili unaotafsiriwa kwamba kinachomuathiri  mtu lazima kipo karibu naye.

Iwe kunguni au chawa, ni lazima wawe kwenye nguo yako mwenyewe ndiyo waweze kukuuma. Maana ya waswahili ni kwamba mtu yoyoye anayekufanyia ubaya, basi ni lazima kwanza awe anakufahamu vizuri.

Wahenga wanaamini kwamba wa mbali hawezi kukufanyia ubaya kwa sababu hakufahamu vema. Adui yoyote anayetaka kushinda vita kirahisi ni lazima kwanza ajue udhaifu wako.

Filamu ya kusikitisha iitwayo 'Sikitu' imeonyesha kila kitu kinachohusiana na hicho. Imechezwa na Kajala Masanja, Hemed Suleiman, Taira Odera, Matra Taimamu, hayati mzee Majuto, Tausi Mgendela, Asha Boko na wengineo wengi.

Hemed na Kajala ambaye amecheza kama Sikitu ni mke na mume. Ni watu wenye uwezo na wanaishi maisha ya kifahari. Sikitu anapatwa na ugonjwa unaomfanya ashindwe kufanya chochote kile. Hemed anaamua kumrudisha nyumbani kwao kwa ajili ya matibabu, pia kupata muda wa kupumzika.

Hata hivyo, Hemed anaingia kwenye penzi na mdogo wa mkewe, Taira. Penzi hilo linakuwa moto moto hadi inakuwa si siri tena. Wazazi pia wanafahamu hilo. Wanawaita na kuwakanya, lakini inakuwa ni kazi bure.

Mwenyewe Sikitu anagundua hilo. Hali yake inazidi kuwa mbaya, anapatwa na mshtuko wa moyo unaosababisha kupooza mwili. Hatimaye anakata roho.

Hemed na Taira wanakwenda msibani, lakini mzee Majuto ambaye ni baba wa mabinti wote wawili, Sikitu na Taira, anamtimua Hemed na mpenzi wake Taira kwa madai wao ndiyo wamesababisha kifo cha binti yake.

Mapenzi ni upofu, yote hayo wanaona ni sawa na wanarejea nyumbani kwao mjini kuendelea na maisha yao ya kawaida. Siku moja isiyo na jina, majambazi wanavamia nyumbani kwa Hemed. Wanataka wamuonyeshe alipoweka hazina ya pesa. Wakati mwenyewe Hemed akisuasua, Taira aliwaonyesha majambazi mkoba wa pesa ulipo.

Kwa mastaajabu, majambazi baada ya kuchukua mkoba ule, wanamkabidhi mmoja wa watu ambao wamewaweka chini ya ulinzi, si mwingine ni Taira.

Ananyanyuka na kuchukua mkoba wa pesa, akamgeukia Hemed na kumwambia hakuwa na mapenzi ya kweli, badala yake alikuwa anazitaka zile pesa tu. Bastola aliyokuwa nayo mkononi ilitosha kumtoa uhai Hemed. Wakati wale majambazi wakidhani watalipwa ujira wao kwa kazi ile, nao wanauawa.

Tayari Taira akajiona mshindi, alichotaka amekipata, akatoka ndani ili atokomee kusikojulikana.

Kumbe mdogo wa Hemed, Matra alikuwa amefika nyumbani hapo na kushuhudia mchezo mzima.

Wakati Taira anatoka, Matra alinyanyua kistuli na kumpiga nacho kichwani, akapoteza maisha hapo hapo. Mkoba wa pesa ukawa mikononi mwa Matra, mdogo wa Hemed ambazo alizipeleka kwa wazazi wake.




## HISTORIA YAWEKWA

# Warembo weusi wavaa mataji, wakumbuka ubaguzi

KWA mara ya kwanza dunia inashuhudia mashindano ya urembo yakitawaliwa na washindi wenye asili ya Afrika na kuondoa dhana ya ubaguzi wa rangi.

Toni-Ann Singh amejishindia taji la 69 la shindano la malkia wa urembo la Miss World na mlimbwende wa Afrika Kusini Zozibini Tunzi, amenyakua taji la Miss Universe.

Katika kile kinachonekana ni historia wanawake wengine weusi wanamiliki mataji ya Miss USA na Miss Teen ambayo yana thamani kubwa katika tasnia ya urembo.

Ushindi wa warembo hao wenye rangi nyeusi umepongezwa na wengi kiasi ambacho mastaa mbalimbali walionekana kushindwa kuzuia hisia zao na kuandika maneno yanayoelezea jinsi walivyokuwa wakijisikia kuona mataji hayo yanaenda kwa wenye rangi nyeupe pekee.

Hata hivyo Miss Universe, Zizibini aliamua kuelezea namna ubaguzi wa rangi ulivyomfanya kushindwa kujiamini na kujiona si mrembo wakati akiwa mtoto.

"Nilikua katika ulimwengu ambao mwanamke anayefanana na mimi, kwa rangi ya ngozi yangu na aina ya nywele zangu, anaonekana si mrembo" aliandika mara baada ya kushinda.

Aliongeza "Ninafikiri ni wakati sasa hali hiyo ikomeshwe."

Zaidi ya wanawake 90 kutoka duniani kote walishiriki kwenye mshindano hayo yaliyofanyika Atlanta nchini Marekani siku ya Jumapili.

Zozibini alimshinda Madison Anderson wa Puerto Rico na Aofia Aragon wa Mexico.

Waliofaulu kuingia fainali ya mashindano hayo waliulizwa maswali kuhusu maada mbalimbali kama vile mazingira, maandamano na mitandao ya kijamii.

Katika swali lake la mwisho, mshiriki Zozibini mwenye miaka 26 aliulizwa kuhusu jambo gani tunapaswa kuwafundisha wasichana wa leo.

"Uongozi ni kitu ambacho kinakosekana kwa wasichana na wanawake kwa muda mrefu si kwa sababu hatutaki, lakini kwa sababu jamii inavyotaka tuwe," alisema.

Zozibini ni mwanamke wa kwanza mweusi kushinda kwenye mashindano hayo tangu Lila Lopes aliponyakua taji hilo mwaka 2011.

Kwa upande wa Toni-Ann aliwafurahisha majaji katika hafla hiyo mjini London baada ya kuimba wimbo wa Whitney Houston ' I Have Nothing', na kujibu maswali tofauti.

Amesema: "Hii ni kama ndoto, nimeshukuru sana. Chochote kile munachokiona ndani yangu, ahsanteni, niko tayari kuanza kazi".

Waliochukua nafasi ya pili walishirikisha Ophely Mezino kutoka Ufaransa na Suman Rao kutoka India.



# Walioacha gumzo kwa kuachana Nigeria

MWAKA 2019 umeshuhudia jinsi baadhi ya mastaa ambao walikuwa wapenzi wakipeana mkono wa kwaheri na kufanya mashabiki wawe na majonzi.

Ifuatayo ni orodha na 'kapo' tano ambazo kuachana kwao kulitingisha na kusababisha habari zao kupamba vyombo vya habari nchini Nigeria.

Waliotajwa katika kapo hizo ni Yvonne Jegede na Abounce Fawole, Osas Ighodaro na Gbenro Ajibade, Ik Ogbonna mkewe Sonia Morales,

Blossom Chukwujekwu na Maureen Esisi na mwisho ni Mofe Duncan na Jessica Kakkad.



## Tacha umeuona upako wa Uche?

MWIGIZAJI mkongwe wa Nigeria, Uche Maduagwu, amemtabiria makubwa mshiriki wa Big Brother Nigeria, Tacha Akide kwa kusema atakuwa na mafanikio ya kiuchumi kama Dangote.

Uche amesema mrembo huyo ameteuliwa na Mungu kwa mwanamke tajiri kwa Afrika kama alivyokuwa bilionea

Aliko Dangote.

Katika shindano hilo ambalo linatoa burudani tosha kwa mashabiki wake, Tacha alikonga nyoyo za watu waliokuwa wakifuatilia kutokana na mikasa yake pamoja na misimamo mikali.


## Chika atambulisha 'Small Chops'

MWIGIZAJI Chika Ike, ametambulisha filamu yake mpya inayojulikana kama 'Small Chops' ambayo itaanza kuoneshwa Juanuari mwaka 2020.

Video ya utambulisho ambayo ina muda wa dakika mbili imewakusanya mastaa wingi wa filamu kutoka Nollywood kama Nkem Owoh, Eucharia Anunobi, Nse Ikpe Etim, Toyin Abraham, Rachael Okonkwo, Lolo na Hafeez Oyetoro.

Filamu hiyo imeongozwa na Roberts Peters na kutengenezwa na yeye mwenyewe Chika Ike kwa kushirikiana na Serah Donalds.





## Wizkid awabwatukia wachungaji feki

MWIMBAJI nyota wa Nigeria, Wizkid amesema yeye hawezi kulikubali kanisa lolote linaoongozwa na wachungaji feki.

Akiweka ujumbe wake katika ukurasa wa Twitter, Wizikid alidai wachungaji feki wameenea maeneo mengi nchini humo na kusababisha watu kupokea mafundisho ya uongo.

"Starboy hawezi kukubali wachungaji wa uongo, nitawapoteza kabisa," ameiandika Wizkid

## Omotola wewe siku nyingine

KITENDO cha mwigizaji Omotola Jalade-Ekeinde kuweka video fupi katika akaunti yake ya mtandao kimemzushia jambo zito.

Msanii mwenzake Eniola Badmus amekuja juu akisema kitendo cha Omotola kuweka video hiyo na yeye kumuondoa hawezi kukisamehe.

Eniola analalamika kwamba wakati inarekodiwa video hiyo yeye alikuwepo eneo hilo, lakini anashangaa ilipowekwa mtandaoni hakuonekana.



**SAFU**

**MIONZI YA SHERIA**



**Na John Juma**
**0716217615**

# Mlinzi anapogeuka kuwa mmiliki nawe kuwa mvamizi

NI muhimu kutahadharishana kuhusu jambo hilo ambalo kwa Kiingereza huitwa 'adverse possession' ni kanuni ya kisheria, inayotokea wakati wavamia ardhi yako baada ya muda wanapohesabika kuwa ni wamiliki halali. Na wanatambuliwa hivyo kisheria na wewe mmiliki halali unageuka mvamizi.

Lakini hoja kubwa hapa si lazima mtu awe mvamizi. Anaweza kuwa mpangaji, au anayekulindia eneo, lengo la hoja ni kutaka kuwatahadharisha wamiliki ardhi hasa wale wanaowaacha watu wawalindie mashamba kwa kukaa bure bila utaratibu maalum. Ifahamike kuwa si kosa mtu kukulindia eneo na wala si kosa mtu kukaa bure kwenye eneo lako, ila ni kosa tena kubwa kufanya hivyo bila utaratibu maalum wa kisheria. Ndipo kugeukana kunapokuja.

Ni rahisi kukugeuka kwa kutumia kanuni hii na wameruhusiwa na mahakama kuwa wamiliki halali.

Kawaida sheria ya ardhi inatambua aina au namna mbalimbali ambazo mtu anaweza kupitia katika kupata ardhi kihalali. Moja ni kununua, kupewa zawadi, kurithi, kutwaa eneo lisilo na mwenyewe, tano ni hii ya kuingia katika eneo kama mvamizi ama vinginevyo na baadae ukabadilika na kuwa mmiliki.

Namna zote hizi ni za kisheria na zinakubalika kama njia halali za kupata na kumiliki ardhi.

**MVAMIZI KUTAMBULIKA**

Mvamizi ni yule anayeingia kiharamu katika ardhi ya mtu mwingine. Inaweza kuwa nyumba, kiwanja au shamba na vilivyomo. Kuingia kiharamu kunafanyika bila ridhaa ya mmiliki na bila ya sababu za kisheria.

Lakini, hata mpangaji au mtu uliyemuacha akulindie eneo anaweza kuhesabika kama mvamizi katika kanuni hii iwapo mmiliki utakosa ushahidi wa maandishi au vinginevyo kuthibitisha kuwa ni mpangaji au ni mtu uliyemuacha akulindie eneo.

Mahakama ya Rufani katika rufaa namba 193/2016 kati ya the registered trustee of the holy spirit sisters Tanzania VS January Kamili Shayo na wengine 136 nayo imeeleza jambo na kuweka misingi yake.

Kesi inaeleza kuwa ikiwa mtu ataingia na kukaa kwenye ardhi yako, iwe nyumba, kiwanja,shamba au vinginevyo kwa kipindi ambacho kinazidi miaka 12 basi mtu huyo mvamizi atageuka kutoka hadhi yake ya uvamizi na kuwa mmiliki halali.

Kwa msingi huu kumbe si salama mtu au watu kuendelea kukaa katika eneo lake bila taratibu maalum zinazotambuliwa na sheria.

Hata hivyo, hoja ya kukaa zaidi ya miaka 12 pekee haitoshi kuthibitisha umiliki bali pia mvamizi athibitishe pia kuwa wakati anaingia hakuwa na ridhaa yoyote kutoka kwa mmiliki, mfano, hakuomba kukaa au kutumia hiyo ardhi, au hakuwa mpangaji, pia athibitishe kuwa hakuwa na haki yoyote kukaa humu mfano sio mtoto au mke wa mmiliki au hakuwa na haki nyingine.

Tunachotaka kusisitiza ni kuwa tuwe makini na watu ambao wanakaa kwenye maeneo yetu kwa mda mrefu na hata wapangaji wa aina hiyo pia.

Namna ya kuweka ardhi yako salama kuepuka, kadhia ya kanuni hiyo, kwanza, yeyote utakayempa ardhi yako kwa ajili ya kulima, kufuga, kuishi ,kupanga au shughuli nyingine yoyote, basi hakikisha mnaandika na kusaini na kuweka picha ikiwezekana na mashahidi.

Mara nyingi walinzi wa maeneo hasa mashamba makubwa na viwanja wamekuwa wakigeuka.

Unaweza kudhani sio rahisi kufanyiwa hivyo na ni masikhara, lakini waliokutwa na haya wanajua nazungumzia nini.

Wapo wengi wametumia kanuni hii kuchukua maeneo ya watu. Na muda huo kama hakuna maandishi mtu anakukana kuwa hukumruhusu aingie bali aliingia mwenyewe baada ya kukuta hamna mtu.

Pili, ni muhimu kuyawekea uzio maeneo yetu kuepuka wavamizi. Kadhalika kuweka vibao hasa kwenye mashamba vinavyokataza uvamizi kwa mfano kibao kinaweza kuandikwa "hairuhusiwi kuingia eneo hili bila kibali maalum".

# Unyanyasaji unavyokithiri sheria, DNA zihusike

**Na Gaudensia Mngumi**

WIKI hii serikali imeshtua Watanzania kwa kutaja vitisho vingi vinavyoliweka taifa roho juu, baada ya kuibua taarifa za kutisha kuwa kuna ongezeko la vitendo vya unyanyasaji kijinsia unaohusisha ongezeko la mimba za utotoni na idadi kubwa ya watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi.

Yapo mengi lakini hili la kuwa na watoto wa mitaani takribani 1,000,000 ni kitisho kingine ambacho taathira yake kitaifa huenda inaweza kulinganishwa na bomu lenye matokeo mabaya.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Afya, Dk. Faustine Ndugulile, idadi ya watoto wa mitaani imeongezeka kutoka 500,000 mwaka 2017 hadi 839,450 mwaka jana .

Anaongeza kuwa si hivyo tu hata tatizo la mimba za utotoni nalo ni hatari kwa vile asilimia 34 ya mabinti wameguswa na changamoto hiyo.

Yote hayo yanaashiria jinsia ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto unavyokomaa nchini.

Pamoja na kwamba taarifa nyingi zinafikishwa polisi watu wakilalamikia unyanyasaji na vitendo vya ukatili hali inayoonyesha kuwapo uhamasikaji mkubwa ndani ya jamii dhidi ya matendo hayo, lakini watoto wengi kupewa mimba kunamaanisha kuwa watu hawajali.

**MIMBA ZA UTOTONI**

Kwa mujibu wa Ndugulile, ni asilimia 34 kwa kila wasichana wenye umri wa chini ya miaka 19, ikiashiria kuwa kwa kila mabinti 100, wasichana 34 wamepata mimba za utotoni.



Baadhi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

Licha ya jitihada za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuwapa mabinti fursa ya kusoma, kulindwa, kuwa na sheria ya mtoto na ile ya makosa ya kujamiiana inaelekea taifa linakuwa sugu .

Mila potofu zimeendelea kuwa kikwazo na kusababisha mimba za utotoni licha ya utetezi wa masuala ya watoto kufanyika kila wakati na jamii inayasikia kwa kushiriki maadhimisho mbali mbali mfano Siku ya Mtoto wa Afrika, Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Siku ya Binti Duniani hata kusoma na kusikiliza taarifa mbalimbali kupitia vyombo vya habari na mitandao.

**SHERIA ZIHUSIKE**

Pamoja na mila potofu mzizi wa tatizo la mimba hizo pengine ulikuwa ni sheria hasa ya ndoa ambayo kipengele cha umri wa kuolewa kuwa miaka 14 kimefutwa na Mahamaka ya Rufani.

Sheria hiyo huenda ilichangia ndoa na ujauzito utotoni.

Hata hivyo kwa sababu imeagizwa kurekebishwa huenda itasaidia kupunguza mimba hizo.

Lakini, Sheria ya Mtoto inahitaji kutizamwa upya ili kuzungumzia na kuweka mkazo Zaidi kumtunza mama kwa vile imeweka kipaumbele kwa mtoto lakini haimjali mama anayetelekezwa.

Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009, sura ya 4(2) inasema "Maslahi ya mtoto yatakuwa ndiyo msingi wa kuzingatiwa katika masuala yote yanayohusiana na mtoto. Aidha, yatakuwa yanashughulikiwa na taasisi za umma au taasisi za binafsi za Ustawi wa Jamii, mahakama au mamlaka za kiutawala".

Sheria hii haijamgusa mama moja kwa moja ambaye ni mzazi wa mtoto. Nivyema mama aangaliwe kisheria kwani iwapo mzazi huyu hatapata msaada ni wazi watoto watatelekezwa na kuongeza idadi ya wanaoishi mitaani.

Sheria iweke mkazo kuwa anayekuwa baba anawajibikaji kwa mama pia kwani wanawake kufukuzwa au ndoa kuvunjika kiholela na talaka za kila siku ndizo zinazowaingiza watoto kwenye maisha magumu mitaani.

Mama apewe kipaumbele, sheria inahitaji marekebisho ili mama anapotelekezwa apate msaada kupitia kumwajibisha na kumwadhibu baba anayehusika na uvunjaji wa sheria kwa kukataa familia yake.

Kwa kutumia mwanya au udhaifu huo wanaume hupuuza kuwatunza watoto na hata kama wataitwa kwenye mashauri ya ustawi wa jamii hawaitikii wito na hawajali na inakuwa ni kawaida kuwatelekeza wanawake na watoto, ambacho huenda ni chanzo cha kuongeza watoto wengi mitaani.

Rushwa nayo imechangia sana watuhumiwa wanaowapa mabinti mimba na kusababisha watoto wa mitaani na mimba za utotoni kuendelea kutesa.

Wazazi na walezi wa wasichana wanapewa fedha ili kuficha kesi, wanapewa rushwa na kuwasaidia watuhumiwa kukimbia na kukwepa kesi.

Inavyoelekea kutoa hela au rushwa si jambo gumu mfano jamii za wafugaji kutoa ng'ombe pengine 20 au hata Shilingi 500,000 ili kukwepa kesi hizo si jambo gumu.

Kwa madereva wa bodaboda nao wanaweza kutoa hela na hivyo usiri huo unaotokana na kula rushwa umesababisha mabinti kupewa ujauzito na kesi zao kuishia kinyemela.

Lakini sasa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imeingilia kati kuchunguza kesi za mimba hizo jambo litakaloleta ufumbuzi.

**DNA**

Aidha, kama serikali ilivyosema inaanzisha kanzidata (database) ya vinasaba kuna haja ya kutunga sheria ya kupima nasaba (DNA) za kila mtu ili zitumike kuwatambua na kuwawajibisha wazazi wa watoto wanaotelekezwa na kuishi mitaani.

Pia, wananchi wafahamishwe kuwa kuna maabara zenye kipimo cha DNA hivyo kukimbia mimba na kutelekeza mtoto si suluhu hatua zaidi zinachukuliwa kuwawajibisha.

## KUELEKEA 2020

# Wanawake wataka rushwa za madera, vilemba zikome

**Na Sabato Kasika**

MWAKA 2020 ni uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani, ikiwa imebakia miezi 10 ili kutimiza takwa hilo la kidemokrasia, ndiyo wakati wa kujipanga na kundi mojawapo linalotakiwa kuwa mguu sawa ni wanawake.

Kinamama wanapofikiria kuingia kwenye uongozi ukiwamo ubunge na udiwani wanakumbushwa kuwa uongozi si zawadi ya kupewa, kwa hiyo wasirubuniwe kwa kofia, chumvi, fulana, madera, khanga na nguo za ndani ili kumchagua kiongozi.

Aidha, wasitoe miili yao ili majina yao yapitishwe kwani huko ni kujidhalilisha na kujinadi kama bidhaa isiyo na thamani sokoni.

Hivi karibuni jijini Dar es Salaam, wadau wa kuhamasisha wanawake kushiriki kwenye uchaguzi mkuu wa 2020 wanakutana katika warsha kujadili masuala kadhaa na 'rushwa ya madera, chumvi, kanga, vilemba' ni moja ya mambo yanayoibuka yakitajwa kuwa kwenye uchaguzi mkuu yanajiri ili kununua kura, hivyo isipewe nafasi.

Waandaji Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kwa kushirikiana na Tanzania Women Fund (Mfuko wa Wanawake) wanawakutanisha kina mama kutoka mikoa mbalimbali, ikiwamo ya Kilimanjaro, Tanga, Mbeya na Dar es Salaam ambao wanaoibua hoja muhimu.

Mshiriki Subira Kibiga, anataja rushwa ya khanga, fulana, kofia, chumvi na nguo za ndani za Sh. 300 kwa wanawake, wakati wa kampeni za uchaguzi ikisema ikomeshwe.

"Kwa vile nayo inatudhalilisha. Wanawake tunapendana, lakini unapofika wakati wa uchaguzi tunatengana huku wengine wakikubali kupokea rushwa hizo, hali ambayo inakwamisha juhudi zetu za kushika nafasi za uongozi," anasema Kibiga na kusema mambo hayo yanawayumbusha wapiga kura.

Anawataka wanawake kuzingatia ajenda ya mwanamke turufu ya ushindi na kwamba kwa kutumia wingi wao wanaweza kupata nafasi nyingi za uongozi iwapo wataungana.



Subira kibiga akichangia mada kwenye warsha hiyo.



Wakili Renatha Seleman akitoa neno.

### RUSHWA YA NGONO

Rushwa hii ni moja ya mambo yanayoibuliwa katika warsha hiyo, kwamba baadhi ya wanasiasa wanaume huwashawishi wanasiasa wanawake wanaotaka uongozi wafanye nao mapenzi, kwa ahadi za kuwasaidia.

"Ukweli ni kwamba mwanamke hana uwezo wa kifedha kama mwanaume na wakati mwingine anashawishiwa eti atoe rushwa ya ngono ili jina lake lipitishwe kuwania uongozi," anasema, Agness Lukanga.

Lukanga anaeleza kuwa mwanamke hatakiwi kuteuliwa kwa rushwa ya ngono, bali kwa uwezo wake wa kuongeza, kwa vile uongozi sehemu ya haki yake, hivyo ajiamini na asikubali kubaishwa.

Mshiriki mwingine Janeth Mawinza, anasema wanawake wasikubali kubebwa katika kuwania nafasi yoyote ile na kama kutakuwa na mambo ya rushwa ya ngono, basi watoe taarifa Takukuru.

"Ukiona kuna dalili za rushwa ya ngono wasiliana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ili kupata msaada tupaze sauti kwani rushwa ya ngono inadhalilisha na inaua," anasema Mawinza.

### ANGALIZO MUHIMU

Pamoja na harakati hizo za kutaka kufikia usawa kwenye nafasi za uongozi, wadau hao wanapewa angalizo, ambalo litawafanikisha kupiga hatua kwenda mbele.

Renatha Selemani ni wakili kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), anasema, ni muhimu kuepuka kuongeza wingi wa wanawake katika nafasi za uongozi bila kuangalia uwezo wa kuongoza.

"Ni muhimu kupata wanawake wenye ushawishi, siyo kuwa na idadi kubwa tu isiyo na manufaa ambayo inakubali viti maalum badala ya kupiga hatua na kuwania nafasi ya kuchaguliwa," anasema Renatha.

Wakili huyo anashauri kuwe na ukomo wa ubunge wa viti maalum, ili wanawake wakapambane kwenye majimbo na kwamba kwa kutumia wingi wao, kuna uwezekano mkubwa wa kushinda.

Akigusia rushwa ya ngono, anasema tatizo hilo lipo na ndiyo maana LHRC, siku zote wanataka sheria iruhusu kuwapo kwa utaratibu wa mgombea binafsi, ili kuepuka tatizo hilo hasa kwa wanawake.

Katika harakati hizo za zinazoambatana na warsha, makongamano na semina kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake ili watambue kwamba wana uwezo wa kusimama na kuwania nafasi yoyote ya uongozi, wanahimizwa wasiogope mfumo dume, ambao umegawa majukumu katika jamii kulingana na jinsia na kuwafanya kuwa watu wa kulea na kutunza wa familia na kazi za nyumbani.

Wanaambiwa nyakati zimebadilika wanalazimika pia kushiriki kwenye masuala ya kiuongozi na kuingia kwenye uwanja wa siasa ili idadi yao iwe sawa na ya wanaume huku njia mojawapo ya kufikia hapo ikitajwa kuwa ni ushirikiano miongoni mwao bila kubaguana kwa itikadi za kisiasa, kikanda wala kikabila.

Katika warsha hiyo ambayo ni mahsusi kubadilishana uzoefu na mafanikio yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa na kuweka mikakati ya kuhamasisha ushiriki wa wanawake, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, waandaji GNP, wanawatahadharisha kuepuka baadhi ya mambo yanayoweza kusabambaratisha umoja wao.

### WANAWAKE WANAPENDANA

Dokta Dinah Mbaga, ni mshauri mtaalam kutoka taasisi ya Tanzania Women Fund, anayewaeleza washiriki kuacha dhana kwamba wanawake hawapendani, kwa vile imeshapitwa na wakati.

"Mkisikiliza hilo itakuwa ni vigumu kufikia kule tunakotaka kwenda, kwa sababu wanaotumia msemo huo wana lengo la kutudhoofisha, hiyo achaneni na nao hiyo, sisi wanawake wote tunapendana," anasema Dk. Mbaga.

Anasema jitihada za kuelekea usawa kwenye uongozi zimeanza kuonekana na kwamba zinahitajika zaidi ili idadi ya wanawake na wanaume katika uongozi iwe sawa.

"Uongozi si misuli, ni akili, busara na hekima, hivyo vyote wanawake wanavyo, kwa hiyo tushirikiane bila kubaguana kwa itikati za vyama na hatimaye tutafanikiwa," anasema.

Anasema, dalili za kufanikiwa kupata nafasi nyingi za uongozi zimeanza kuonekana lakini wanahitaji kuongezeka kuwa na madiwani na wabunge zaidi kwa vile taifa linahitaji viongozi wanawake na wanaume.

### USHIRIKI MDOGO

Mwenyekiti wa TGNP Asseny Muro, anakirejea ripoti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anasema, katika uchuguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2014, idadi ya wanawake waliochaguliwa kuongoza mitaa, vijiji na vitongoji ilikuwa ndogo.

Anasema, katika uchaguzi huo wenyeviti wa mitaa waliochaguliwa ni 3,929, kati yao wanawake wakiwa ni 435, na waliochaguliwa nafasi za mwenyekiti wa vijiji ni 12,275, kati yao wanawake wakiwa ni 223.

"Kwa upande wa wenyeviti wa vitongoji, waliochaguliwa ni 64,691, wanawake ni 3,482 idadi hii ni ndogo na bado tunasubiri taarifa ya uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka huu," anasema Muro.



Dk. Dinah Mbaga akizungumza kwenye warsha hiyo.



Baadhi ya wadau wakiwa kwenye warsha hiyo. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**



Sehemu ya bunge la wanafunzi wa Shule ya Msingi Kilindoni wilayani Mafia, wakisikiliza na kujadili masuala ya ustawi na changamoto za watoto. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI.**

# Wazazi zisikieni sauti hizi za watoto wenu

**Na Mwandishi Wetu**

AKIWA na umri wa miaka 17 Maua Mapani anayeishi mtaa wa Mzambarauni wilayani Mafia ni mama wa watoto wawili, anayeeleza kuwa mwanae wa kwanza alijifungua akiwa na miaka 13 na anakiri kuwa yeye ni tunda la utoro shuleni na ndoa za utotoni.

Aliachishwa shule baada ya kupewa ujauzito na fundi 'mekanika' aliyekuwa anafanyakazi kwenye gereji jirani na nyumbani kwao, ambaye pia leo ndiye mumewe.

Akiwa na mwili mdogo na kimo kinachoonyesha udumavu, anasema ni mjamzito anayetegemea kupata mtotto wake wa tatu Februari mwaka ujao 2020.

Mapema mwezi uliopita anakutana na Nipashe kisiwani Mafia, akieleza kuwa anapata riziki kwa kufanyakazi kwenye nyumba za baadhi ya watu wanaompa kazi za kufua na kusafisha nyumba na kuosha vyombo.

Lakini, wakati mwingine anauza matunda ya msimu kama maembe, mapapai na matikiti ili kupata riziki kwa ajili ya malezi ya watoto wake.

Anapoulizwa vipi kuhusu mumewe, anasema ana wake wawili wakati akimuoa alipomwachisha shule binti huyo ambaye wakati huo alikuwa na miaka 14. Anasema Licha ya kuwa na miaka 42 mumewe huyo, hamsaidii kitu wala hana malezi kwa watoto wao licha ya kwamba hajampa talaka.

"Ana wanawake wengine wawili na jumla mimi na wenzangu tuna watoto 11," anasema Maua aliyepata mimba kutokana na kutumikishwa kazi za jioni za kuuza samaki mitaani ikiwamo kwa wafanyakazi wa gereji hiyo, alikokuwa akifanyakazi mumewe huyo.

Changamoto hiyo ya ngono, mimba na ndoa utotoni, kuolewa na waume wazee kama ilivyomuathiria Maua (japo si jina lake halisi) inawakabili wasichana wengine wengi katika mikoa mbalimbali na si Mafia pekee.

Kisiwa hiki kilichoko mkoani Pwani tatizo la utoro shuleni, mimba na ndoa za utotoni ni changamoto inayowaibua wadau wa utetezi wa msichana, kuchukua hatua, likiwamo Shirika la kimataifa la ActionAid, ambalo limeanzisha mradi Stop Violence Against Girls in Schools (SVAGs), au ulinzi wa wasichana

Mratibu wa ActionAid, Wilaya ya Mafia, Samuel Mesiaki, anasema kazi mojawapo inayofanyika kukabiliana na unyanyasaji wa mabinti wilayani humo ni kuanzisha mabunge ya wanafunzi shuleni.

Katika mabunge hayo wanafunzi wanajengewa uwezo na kuwezeshwa kujiamini, kujisemea na kuzungumza masuala yanayohusu ustawi wao kijamii, kitaaluma na kulindwa dhidi ya uovu kama ukatili wa kijinsia unaohusisha utumikishwaji, ubakaji, mimba na ndoa za utotoni.

Katika ziara ya wanahabari kisiwani humo iliyoandaliwa na taasisi hiyo, Mesiaki, anawafikisha wanahabari kwenye Bunge la Watoto wa Shule ya Msingi Kilindoni, wanaopaza sauti zao kufikisha ujumbe kwa jamii kuwa kinachosababisha mabinti kunyanyaswa kingono, kuozwa utotoni na kutoroka shuleni ni pamoja na kutumikishwa kwenye kazi za nyumbani na kulazimishwa kufanyabiashara hadi saa 4:00 usiku.

Aidha, wanapokusanyika kama bunge la shule na kufanya mijadala mbele ya wadau mbalimbali wakiwamo wanahabari, wanaeleza kuwa wanalazimishwa kwenda kwenye mitumbwi na boti baharini kuomba ili kuzipatia familia zao riziki licha ya kwamba muda huo walitakiwa kupumzika au kujisomea ili kujiandaa na masomo siku inayofuata.

Moja ya sauti za bunge hilo ni ile inayotolewa na mwanafunzi wa darasa la tano Juma Mussa, anayeeleza kuwa kuwatumisha watoto kunawasababishia matatizo ya kiafya .

Anaeleza kuwa katika umri wao mdogo watoto hao wa kisiwa cha Mafia wanadumazwa na kazi kwani wanatumia nguvu zao nyingi kwenye kazi badala ya taaluma.

Saada Khatibu, mshiriki wa bunge hilo, anasema watoto wanatumiwa kwenye mambo ambayo hayawasaidii kwa mfano kufanyishwa kazi ngumu badala ya kulindwa wasinyanyaswe , kupata haki zao za msingi na kupendwa.

Anawalaumu wazazi kuwapa jukumu la kufanyabiashara usiku kuuza vitafunwa, samaki na matunda hadi saa 4:00 usiku na kusababisha kushindwa kusoma.

Gloria Tesha mwanafunzi wa shule hiyo, anaongeza kuwa wanafanyakazi usiku hawali chakula kwa wakati, kupumzika wala kusoma hivyo wanapoteza muda, masomo na hata haki yao ya kukua.

Zuhara Omary, anazungumza kwenye bunge hilo akieleza kuwa biashara za kwenda kwenye boti kuuza bidhaa nazo ni tatizo kwa wanafunzi wa Mafia wakiwamo mabinti ambao hilo ni eneo jingine la kupotezwa kutokana na wanaokutana nao kukosa maadili na kuwadhulumu kingono.

"Wakati mwingine mzazi anampa mwanae kazi ya kuvua kwa kutumia mshipi (kamba na ndoano). Badala ya kumwelekeza kusoma anamtuma kuvua bahari tena jioni ni hatari kwake kwani akizoea kwenda baharini anapoteza muelekeao na mapenzi ya elimu." Anasema Zuhura.

Anasema wazazi wao hawazijui haki za watoto, kwa mfano wanawatumikisha kama watu wazima na wengine wanapofanyabiashara wanaanza kuzoea pesa kiasi kwamba hawapendi tena kusoma. anasema Khalifan Khatibu, anayesoma darasa la tano.

"Wazazi hawajui haki hizo ndiyo maana huwatuma kufanyabiashara usiku bila kujali kuwa kwa binti ni chanzo cha kubakwa, kupata mimba na kuambukizwa maradhi." Anakumbusha.

Mabinti hawa wanarubuniwa na watu wenye pesa wanaowaona kwenye biashara hizo kwa kuwapa pipi na zawadi ndogondogo na matokeo yake hutumbukia kwenye mitego ya mimba.

"Kuna baadhi ya wazazi na walezi wanawashauri wasichana wa darasa la sita na saba wajifelishe ili wasiendelee na masomo . Anawashauri kufanya hayo ili waolewe,"anasema Faraja Abdallah.

**BUNGE LIMEWASAIDIA**

Wanafunzi hawa wanasema bunge la shule limewasaidia kufahamu mambo mbalimbali zikiwamo haki za watoto, sharia ya mtoto pamoja na kutumika kuwasaidia baadhi ya watoto mitaani wanaonyanyaswa.

Wanasema wamefahamu haki zao na changamoto na sasa wanataka elimu na maarifa yapelekwe kwa wazazi na walezi zaidi ili wabadilike na kuwalinda watoto, anasema Gloria Tesha.

Wanaeleza kuwa wamefahamu namna simu zinavyotumika kuwahadaa mabinti ambao wanapewa simu halafu zinatumiwa na wanaume kuwatumia fedha, kuwasiliana nao na baadaye anamfuata na 'kudai chake.'

Wanafunzi hawa wanataka pamoja kuzingatia sheria, jamii zibadilike na ziache kuwatumikisha watoto kwani kazi ngumu huwadhoofisha miili, huwaingiza majaribuni, huwachosha na kwa ujumla humwingiza mtoto kwenye matatizo badala ya kumpa nafasi ya kutimiza ndoto zake.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 25 00)



Dondoo: Kulia
1. Moyo wa wema
6. Buriani, radhi
7. majivuno, ndweo 9. Eleza
12.Nyumba ya Wasomalia
17.Tando, vyero
18.Sampuli
20.Huvuta vitu asili ya chuma
22.karo ya shule
24.Safika
25.Maisha ya starehe
27.Sura katika kitabu 28.Kubali
30.Mapango yaliyoko Tanga
32.Shauku ya kitu
33.Chimbuko
34.Mkokoteni
35.Hutoa mawazo

Dondoo: Chini
1. Toa uamuzi kwenye kesi
2. Mwendesha ndege
3. Mama wa Yesu Kristo
4. Mzazi wa kike
5. Hongo 8. Zawadi, kipawa
10.karatasi inayotiwa barua
11.Sehemu ya juu ya ardhi
13.Madhumuni, makusudio
14.Kwa haraka na kwa nguvu
15.Shika shavu kwa huzuni
16.Mji mkuu wa Uturuki
19.Saidia 21.Mzaha
23.Milele 24. Ponda nafaka
24.Sanduku kubwa la wima
26.Malipo ya mkosaji 29.Labda
31.Neno la Scotland "kila"

### Jibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | A | R | A | S | I | | U | M | I | Z | W | A |
| U | | W | | H | | M | | A | | I | | M |
| N | Y | A | S | A | L | A | N | D | | D | | B |
| U | | N | | K | | R | | A | K | I | L | I |
| N | I | D | H | A | M | U | | R | | W | | W |
| U | M | A | | Z | | D | H | A | M | A | N | A |
| | A | | K | U | M | I | | K | | | Y | |
| | M | | | L | | O | M | A | N | | U | |
| S | U | M | B | U | A | | T | | Y | | M | |
| H | | T | | | D | | U | K | U | M | B | I |
| O | K | O | T | W | A | | M | | M | T | A | A |
| K | | T | | | | M | W | I | B | A | | S |
| A | G | O | S | T | I | | A | | U | A | N | I |

## LICHA YA MAFANIKIO:

# Upimaji, urasimishaji ardhi bado unahitajika Morogoro

Na Mashaka Mgeta,
MOROGORO



Ofisa Programu wa Mtandao wa TALA, Jamal Juma (kushoto mbele), akikusanya maoni ya wakazi wa Kijiji cha Isiyaga wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro hivi karibuni. **PICHA: MASHAKA MGETA.**

WANANACHI wa Morogoro walionufaika na mradi wa Kuwezesha Umilikishaji Ardhi (LTSP) kwenye wilaya za Ulanga, Kilombero na Malinyi uliofanywa na wadau wa mtandao wa utetezi wa masuala ya ardhi (Tala) na serikali, wanaposhuhudia mradi huo ukielekea ukingoni wanakuja na ombi kwa serikali.

Wanafurahia mafanikio mengi kama utatuzi wa migogoro, utambuzi wa mipaka na upatikanaji haki kwa wanawake kumiliki lakini wanasema zipo baadhi ya changamoto kama baadhi ya maeneo kutopimwa na wamiliki kukosa hati miliki za kimila na pia kutofanikiwa kupata mikopo kwa kutumia ardhi kuwa ni mambo yanayohitajika kuwekwa sawa.

Vijiji kama Mwaya na Libenanga wilayani Ulanga mipaka yake ina mgogoro ambao kila upande unalitambua eneo hilo kuwa sehemu yake, pia vitongoji vya Ume na Ifuma vilivyoko Mwaya mjini, vinatajwa kutopimwa kutokana na mgogoro wa mpaka.

Mwenyekiti wa kitongoji cha Mwaya Mjini, Samson Ngusi, anasema kijiji cha Libenanga kilikuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi tangu mwaka 2013, uliowawezesha kupimiwa maeneo yao isipokuwa lenye mgogoro, wakati Mwaya haijakamilisha mchakato wa kuwa na mpango huo.

"Kwa hiyo ilikuwa rahisi maeneo ya Libenanga kukamilisha upimaji, urasimishaji na umilikishaji ardhi kuliko ilivyokuwa kwa Mwaya," anasema.

Wakati hali ikiwa hivyo, aliyekuwa mjumbe wa serikali ya kijiji cha Mwaya na hivyo kushiriki upimaji maeneo, Bakari Ndimbo, anasema wajumbe kutoka kijijini humo walilazimishwa kusaini nyaraka za mipaka bila ridhaa yao, hivyo sehemu nyingine ikaonekana kuwa upande wa Libenanga.

"Tulipigiwa simu kwenda kutambua mipaka, hatukuwa na uelewa unaostahili, lakini baada ya kuzungumza, tukalazimishwa kusaini nyaraka za mipaka na kama tusingefanya hivyo wangetunyima posho," anasema.

Pia anasema mpimaji mipaka alikuwa mjamzito ambaye muda mwingi alibaki ndani ya gari pasipo kufika kwenye maeneo husika, na akajaza fomu kwa kutumia taarifa zilizotokana na vipimo vya GPS.

Eneo jingine ni lile la kijiji cha Siginali linalopakana na eneo la uhifadhi (WMA) la Iluma wilayani Kilombero. Kijiji hicho kinadai eneo lake 'limemegwa' kutoka hekta 2,170 za awali kufikia 530.

Mgogoro huo ulijadiliwa katika ngazi tofauti za msingi na sasa umefikishwa kwenye uongozi wa serikali wilayani Kilombero unaposubiriwa kupata ufumbuzi.

Maeneo mengine yanayotajwa kutopimwa kwa kuwekwa kwenye mabadiliko ya kuwa Mji Mdogo ni kwenye vijiji vya Malinyi, Kipingu, Lugala, Mchangani na Makelele wilayani Malinyi.

Pia, vitongoji vya kijiji cha Misegese mbavyo sehemu ya ardhi yake ipo ndani ya mpango mji ni Kigamboni, Mwembeni na Nakatele, wakati vile vya Misegese, Kilolelo na Sarago vipo nje ya mpango huo hivyo vinahitaji kumilikishwa hati miliki za kimila.

Kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba maeneo yanayoangukia kwenye mpango mji hayawezi kuwa sehemu ya mradi wa LTSP.

**MIKOPO**

Moja ya faida za hati miliki za kimila zinazoshawishi mradi huo kuwafikia watu 'walioachwa pembeni' ni matumizi yake hati kama dhamana katika kupata mikopo kwenye asisi za kifedha zikiwemo benki.

Hata hivyo, matokeo ya baada ya kupatikana hati hizo yanaonyesha kuwa fursa hiyo imekuwa ngumu kutokana na kukosekana mfumo wa kuwaunganisha wamiliki ardhi na asasi hizo.

Pia, baadhi ya wamiliki waliofika kwenye asasi hizo kutafuta mkopo kwa kutumia hati miliki za kimila kama dhamira, hawajafanikiwa.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Signali wilayani Kilombero, Elpidius Ndumba, anasema pamoja na changamoto hiyo, wapo wachache waliofanikiwa kuziweka rehani hati miliki zao na kupata mikopo, wakiwamo mafundi walionufaika kwa kupata Sh. 300,000 kwa kuweka rehani hati-miliki ya shamba lake kijijini hapo.

Mwaija Lyawala, mkazi wa kijiji cha Nkongo wilayani Ulanga, anasema elimu sahihi kuhusu matumizi ya hati miliki hizo bado haijawafikia, na hivyo kuwafanya waendelee kuzihifadhi ndani.

Pia anasema wengine wana hofu kwamba kama watatumia hati hizo kupata mikopo, maeneo yao yatauzwa pindi wakishindwa kulipa kwa wakati.

Kwa upande wake, Temeleta Wongo, anatajwa kuwa na eneo la ekari mbili alipata mkopo wenye thamani ya Sh.200,000 kwa kuiweka dhamana hati miliki yake kwa kampuni inayoelekezwa na asasi nyingi za ki-fedha kuwa na makubaliano na wanavijiji.

Ofisa Mtendaji wa kijiji cha Chirombola wilayani Ulanga, Novatus Ntyangiri, anasema jitihada za kuwaunganisha wamiliki wa ardhi na asasi za kifedha zinakwamishwa na matakwa ya kuwataka wajiunge kupitia kampuni hiyo ambayo viongozi wake hawakupatikana kutoa maelezo.

Kwa mujibu wa Ntyangiri, wamiliki wa hati hizo wameshawasiliana na benki kadhaa za biashara na kupata maelekezo hayo, pamoja na kutakiwa kuendeleza maeneo yao ili kuyapandisha thamani.

Tofauti na maeneo mengi kwenye wilaya hizo, kijijini Siginali kunatajwa kuwapo mkulima mmoja mkazi wa Dar es Salaam, aliyepewa utambulisho na ofisi ya mtendaji wa kijiji kupata barua ya utambulisho ili akachukue mkopo wa trekta kwa dhamana ya hati miliki ya kimila.

Hata hivyo mwanakijiji cha Nyamwezi wilayani Kilombero, Bonifas Nagireki, anasema aliwasiliana na benki kadhaa ili atumie hati miliki za kimila kukopa lakini hakufanikiwa kwa madai kuwa ardhi yake haina thamani.

Taarifa hiyo inawakatisha tamaa wakazi wengine wa kijiji hicho kwa kuamini kwamba kama Nagireki, mfugaji mwenye kumiliki eneo kubwa la ardhi ameshindwa kupata mkopo, haiwezi kuwa rahisi kwa wenye maeneo madogo kukopeshwa.

**HAKI ZA WANAWAKE**

Wanawake wa kijiji cha Sofi Majiji wilayani Malinyi, wanasema awali, ilikuwa jambo la kawaida kwa jamii hiyo kuwanyima haki ya kumiliki ardhi, na kwamba hata wanandoa walipotengana, mwanamke aliondoka pasipo kunufaika na rasilimali hiyo.

Grace Najalamoto, anasema hali hiyo ilizidisha ubaguzi na dhuluma kwa wanawake hasa walioachika, pasipo kujali wanavyoshiriki 'kuzalisha' mali ya familia hasa ardhi.

Simon Mazee, mkazi wa kijiji hicho anatoa mfano kuwa kabla ya LTSP, ardhi ya ukoo wao ilikuwa inasimamiwa na baba yake mzazi, ambaye pia alikuwa na uamuzi wa mwisho kuhusu matumizi yake.

Anasema baada ya utekelezaji wa mradi huo, shangazi zake walitambuliwa kuwa wamiliki wenye haki na uamuzi, kupitia hati miliki za kimila zenye majina na picha zao. Naye Rock Juma, anasema familia yao yenye watoto saba, watatu miongoni mwao wakiwa wanawake, wamemilikishwa ardhi ya familia tofauti na awali ambapo umiliki ulikuwa chini yake, akiwa mtoto mkubwa wa kiume.

"Zamani ningeweza kufanya uamuzi wowote ikiwamo kuuza ardhi pasipo kuwashirikisha ndugu zangu wa kike, lakini kwa sasa siwezi kwa sababu nao ni sehemu ya wamiliki wanaotambuliwa kupitia hati miliki ya kimila," anasema.

Nicolaus Siti kutoka Siginali wilaya ya Kilombero, anasema hivi sasa wanawake wanatambua namna ya kukabiliana na vitendo vya unyanyaswaji kwa masuala ya ardhi na haki nyinginezo.

Anatoa mfano wa mkazi wa eneo la Kipingu, maarufu kama Mama Kadege, alipowahi kutumia haki yake kuzuia uvamizi wa sehemu ya ardhi yake dhidi ya mtu aliyekuwa akitumia tingatinga kusafisha ili aichukue.

"Tingatinga lilimsukuma Mama Kadege hadi akaanguka na kumjeruhi, ila kutokana na kutambua haki zake, alikwenda kwenye vyombo vya sheria na akalipwa haki zake zote," anaeleza mmoja wa wakazi wa Siginali.

Msaidizi wa sheria wilayani Malinyi, Martha Nandika, anatoa mfano wa mkazi mmoja wa kijiji cha Biro , aliyemmilikisha ardhi binti yake pasipo kumjulisha mkewe, aliingia kwenye mgogoro uliotatuliwa kwa kutumia hati miliki za kimila.

Licha ya kumrithisha na kumwandikisha binti yake katika umiliki wa ardhi, mzazi huyo, anadaiwa kutaka kulitumia eneo hilo kwa matumizi yake binafsi, lakini binti yake alitumia hati hiyo kuweka pingamizi na hivyo kuiokoa ardhi yake.

## HABARI KIMATAIFA

# Trump atamba hahofii kesi

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ametaka kesi inayomkabili ya matumizi mabaya ya mamlaka kuwasilishwa haraka katika bunge la Seneti.

Kesi hiyo inakabiliwa na mgogoro kati ya wabunge wa Democrats na Republicans kuhusu siku ya kuanzishwa.

Siku ya Jumatano, bunge la wawakilishi nchini humo lilipiga kura ya kutaka kumuondoa madarakani kwa madai ya utumizi mbaya wa mamlaka na kulizuia bunge la uwakilishi.

Lakini Democrats wamekataa kuanzisha kesi hiyo, wakidai kwamba bunge la seneti linadhibitiwa na Republicans ambao wamekataa mashahidi na kwamba haliwezi kufanya kesi ya haki.

Idadi ya wanachama wa bunge la seneti inaonyesha wazi kwamba Trump huenda akaondolewa mashtaka hayo.

**Mchakato wa kumuondoa madarakani kiongozi huyo umechochewa na migawanyiko ya mabunge hao mawili kulingana na vyama vyao.**

Mchakato wa kumuondoa madarakani kiongozi huyo umechochewa na migawanyiko ya mabunge hao mawili kulingana na vyama vyao.

Mashtaka yaliowasilishwa dhidi ya Trump yanafuatia madai kwamba rais huyo aliishinikiza Ukraine kuchunguza habari kuhusu mpinzani wake wa Democrats Joe Biden na mwanawe wa kiume Hunter, na baadaye akakataa kushirikiana na uchunguzi wa bunge kuhusu swala hilo.

Katika msururu wa jumbe za twitter, rais huyo aliwashutumu wabunge wa Democrats kwa kukataa kuendelea na kesi hiyo kwa kuwa kesi yao ilikuwa mbaya.

"Baada ya Democrats kukataa kunipa haki yangu bungeni, bila kuwa na wakili bila mashahidi, sasa wanataka kuliambia bunge la seneti jinsi ya kuendesha kesi hiyo," aliandika katika Twitter.

Katika ujumbe mwingine aliandika "Kwa kweli hawana thibitisho la chochote, Na pia hawatakuwapo .Nataka kesi hiyo kufanyika sasa hivi!"

Rais alisema Democrats hawamtaki Adam Schiff, ambaye aliongoza mchakato wa kesi hiyo , familia ya Biden na wala mfichuzi wa CIA ambaye alisababisha kufanyika kwa uchunguzi huo kutoa ushahidi.



Ili kesi hiyo kuanza, bunge la uwakilishi linalodhibitiwa na Democrats ni sharti liwasilishe nakala za kesi hiyo kwa bunge la seneti.

Lakini spika wa bunge la uwakilishi Nancy Pelosi amekataa kufanya hivyo hadi pale sheria za kesi hiyo za seneti zitakapokubaliwa na Democrats.

Kiongozi wa Republican katika bunge la seneti Mitch McConnell , ataamua masharti ya kesi hiyo na Democrats wanamtaka kutoa maelezo kuhusu mashahidi na ushahidi utakaoruhusiwa.

McConnel amekataa kukubaliana na Democrats kwa kusema "Tunasalia katika mkwamo," Bunge la Seneti lina idadi kubwa ya wabunge wa Republican katika bunge hilo. Wabunge 53 wa Republican katika bunge hilo lenye viti 100 na kwa kura hiyo kumuondoa madarakani rais Trump itahitaji kuungwa mkono na thuluthi mbili ya wabunge. **BBC**

## Ukahaba sasa ruksa Nigeria

**ABUJA,** NIGERIA

MAHAKAMA kuu jijini Abuja imetangaza kwamba ukahaba sio uhalifu nchini Nigeria.

Uamuzi huo umejiri katika kesi iliyokuwa inashirikisha wanawake 16 waliokamatwa kwa kufanya ukahaba.

Ni mara ya kwanza kwa mahakama ya Nigeria kuamuru kuhusu uhalali wa biashara hiyo ambayo inazidi kuonekana kuwa uhalifu mkubwa miongoni mwa mataifa mengi Afrika.

Jaji Binta Nyako wa mahakama hiyon alisema kwamba hakuna sheria inayoharamisha ukahaba nchini humo.

Kesi hiyo iliowasilishwa mwaka 2017 ilifuatia kukamatwa kwa baadhi ya wanawake mjini Abuja kwa madai ya kushiriki katika biashara hiyo.

Licha ya serikali ya taifa hilo kudai kwamba wanawake hao ni wahalifu, lakini mahakama ilipinga hilo na badala yake kuagizia kwamba walipwe fidia.

Wakili mmoja aliyekuwa akiwawakilisha wanawake hao Babatunde Jacob, aliambia BBC kwamba mahakama iliamuru vyombo vya usalama kukiuka haki za wateja wake wakati walipovunja na kuingia katika nyumba zao na kudai kwamba wanawake hao walikuwa makahaba.

Wataalam wa sheria wanaamini kwamba uamuzi huo utakuwa na athari kubwa kwa taifa hilo lenye idadi kubwa ya watu barani Afrika.

Kukamatwa kwa makahaba na vyombo vya serikali ni kitu cha kawaida. Katika msako mmoja mnamo mwezi Mei mwaka huu, zaidi ya wanawake 60 walikamatwa kwa kudaiwa kushiriki katika biashara hiyo.

Wanawake hao walidai kwamba, walinyanyaswa, kupokonywa fedha zao kwa nguvu na kuaibishwa hadharani. **BBC**



Malkia Elizabeth wa Uingereza, akiingia ndani ya ukumbi wa Bunge kulizindua baada ya kufanyika uchaguzi mkuu ambao ulimrudisha kwa kishindo Waziri Mkuu Boris Johnson mwez i huu. **PICHA: BBC**

## UN yaongeza muda wa ulinzi Congo DR

**NEWYORK,** Marekani

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN), limeidhinisha nyongeza ya mwaka mmoja wa kulinda amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, wakati huo huo ikipunguza idadi ya wanajeshi na kuongeza maofisa wa polisi.

Azimio lililowasilishwa na Ufaransa, ambalo pia linaweka mkakati wa kuondoka nchini humo lilikubaliwa kwa hiari na wanachama 15.

Balozi wa Afrika Kusini, Xolisa Mabhongo, akizungumza kwa niaba ya washirika watatu wa Umoja wa Afrika, alipongeza mpango huu na kwa kusema ni muhimu kujiondoa kwa Jeshi la Ulinzi wa Amani la UN Congo au Monusco kwa msingi wa mabadiliko baada ya kufikiwa mafanikio katika mkutano wao.

Kwa upande wake, mwakilishi wa Kongo, Paul Empole Losoko Elambe, amesema wazo la kulenga vikosi vya Monusco katika majimbo sita ambayo uwepo wa vikosi unadhaniwa kuwa ni muhimu ni sawa na hitaji la serikali la kujikita zaidi katika majimbo ambayo yana kiwango cha juu cha vitisho.

Kikosi cha jeshi la umoja wa maifa Munusco kitapunguzwa kutoka askari 16,875 hadi 14,660.

Katika rasimu hiyo, Baraza la Usalama linataka Sekretarieti ya Umoja wa mataifa izingatie kupunguzwa zaidi kwa kiwango cha kupelekwa wanajeshi kwa kuzingatia mabadiliko mazuri ya hali ya nchini Kongo, hasa katika mikoa ambayo inakabiliwa na tishio la vikosi vya wahalifu wenye silaha. **DW**

## Johnson awasilisha mpango kujitoa Brexit

**LONDON,** Uingereza

BUNGE la Uingereza litayapigia kura makubaliano ya kujitoa nchi hiyo katika Umoja wa ulaya yanayojulikana kama Brexit.

Kabla ya hapo waziri mkuu Boris Johnson anatarajiwa kuwasilisha mswada huo bungeni.

Wakati huo huo kiongozi huyo anataka uondolewe uwezekano wa kurefushwa kipindi cha mpito ambacho kimsingi kimepangwa kumalizika mwisho wa mwaka 2020.

Idadi kubwa ya wabunge wataupigia kura makataba huo kufuatia ushindi wa chama chake katika uchaguzi uliopita wa bunge.

Spika wa bunge Jacob Rees-Mogg, alisema serikali inataka sheria hiyo mpya iidhinishwe hadi ifikapo Januari tisa inayokuja. **BBC**


# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

## JUMBA JEKUNDU- 32

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




**Na Adam Fungamwango**

KAMA kawaida yake, ukiona mama Gombea anapitapita kwenye nyumba za jirani zake ujue kuwa kitu. Anapeleka umbea, au anatembeza sare za ngoma.

"Mama Kadili habari za asubuhi?" Alisalimia akiwa nje, baada ya kutomuona mtu yoyote ndani.

"Nzuri tu, mbona asubuhi asubuhi mama Gombea kwema huko, maana wewe mwenzangu, una mambo wewe."

"Aka mwenzangu nimepita tu kukusalimia, nakwenda kudai madeni yangu, maana kuna wengine lazima uende saa hizi, maana ikishafika saa tatu au nne, huwakuti, wameshakimbia majumba yako, chezea madeni wee."

"Hebu toka kidogo shosti nakuhitaji."

Mama kadili alijua kabisa kuna ubuyu. Kwa sababu mama Gombea anajulikana sana mtaani kwa kazi hiyo. Hakuna ambacho kinampita. Hakuna ambacho hakifahamu.

"Huyo mwanao Kadili yupo?" Mama Gombea aliuliza baada ya mwezake kutoka nje.

"Amelala."

"Na huyo mchumba wake mtarajiwa?" "Ametoka kwenda kuwasaidia mawifi zake kuuza supu barabarani."

"Shoga jana kwa macho yangu haya mawili, nimewaona."

**Aka mwenzangu nimepita tu kukusalimia, nakwenda kudai madeni yangu, maana kuna wengine lazima uende saa hizi, maana ikishafika saa tatu au nne, huwakuti, wameshakimbia majumba yako, chezea madeni wee.**

"Nani mama Gombea, mbona unanitisha?"

"Huyo mwanao binti ya kaka yako."

"Eliza?"

"Nani mwingine. Huyo huyo, pamoja na Meze. Nimewaona usiku pale dukani. Nimekuja kukwambia shoga kuwa kumbe Meze anamzunguka mwenzake, anatembea na Eliza. Kwa macho yangu haya mawili nimeshuhudia."

"Uliwashuhudia wanafanya nini we mama Gombea, siyo wamesimama tu mtu na shemeji yake ukawasingizia." Mama Kadili alijaribu kupoza joto, lakini yeye mwenyewe akiwa ametaharuki.

"Yaani nini unanifanya mtoto mdogo ee? Mtu akisimama na shemeji yake sijui na mtu na mpenzi wake sijui.

Maongezi yao yote na jinsi walivyokuwa wakishikana, inaonyesha kabisa kuwa wala si mtu na shemeji yake. Kuna kitu."

"Basi mama Gombea ishia hapo hapo." "Basi mama habari ndiyo hiyo, mwambie mwanao Kadili kuwa rafiki yake si rafiki, anamzunguka."

**********************************

"Nataka uniambie Eliza, Meze ukoje naye?" Mama Kadili aliuliza swali akiwa amekasirika.

Alikuwa ameitisha kikao kati yake, Eliza na Kadili. Mwenyewe alikiita kikao cha siri ili kuweka mambo sawa. Hakutakiwa yoyote afahamu zaidi yao tu.

"Ni shemeji yangu." Alijibu kwa wasiwasi akiwa hajui nini kimetokea.

"Jana umeonekana na Meze, lakini inaonekana kabisa kuwa hamkuwa kwenye hali ya kawaida. Mlikuwa ni kama mtu na mpenzi wake."

"Siyo kweli shangazi. Jana kweli nilienda dukani usiku kununua mafuta ya kuchomea chapati asubuhi, lakini nilikuwa nakwenda kumuangalia Kadili kwa sababu sikumuona mchana kutwa." Alijibu Eliza akiwa ameinamia chini.

"Huna uhusiano wowote wa Meze wewe? Na kwa nini unakwenda kwenye maduka ya watu usiku?"

"Shangazi si nimekwambia kuwa nilikwenda kununua mafuta ya chapati? Halafu wala hakuna lolote baya tuliloongea, yeye alikuwa ndani ya duka na mimi nje, halafu pia nilikwenda kumuulizia Kadili, hapo nimefanya ubaya gani?" Kumbukumbu ikamrudisha nyuma Eliza akawa anakumbuka alichokuwa akizungumza na Meze.

"Kadili hata mimi sijamuona muda mrefu sasa." Alijibu Meze na kuongeza.

"Mimi nilidhani uko naye nyumbani huko."

"Hapana aliondoka muda mrefu sana, mpaka saa hizi inafika saa tatu usiku bado hajaonekana." "Eliza wacha wivu, mumeo mtarajiwa atarudi tu, au unadhani yuko na wanawake wengine?' Alihoji.

"Mhh, hapana usalama wake muhimu kwanza."

"Siyo wivu bibie?"

"Hapana sina wivu kwa sababu sidhani kama rafiki yako ananipenda hasa."

"Kwa nini?"

"Huo unafiki, hata wewe unajua hilo. Kuna mtu anampenda, ndiyo anayemsumbua, na mimi nimekuwa kama mbadala tu, ikishindikana kabisa ndiyo anioe mimi."

"Sasa hilo linakukwaza?"

"Sana tu, nimekubali kwa sababu wanaotaka hili litimie ni shangazi yangu, mama yake Kadili na baba yangu mzazi mzee Tengeneza, kaka yake shangazi, vinginenvyo nisingekubali."

"Ila kuolewa unataka?"

"Meze, hakuna mwanamke asiyekubali kuolewa. Lakini anataka kuolewa na mwanaume anayempenda na kumjali, lakini kwangu mimi kwa Kadili ni kama spea tairi ambalo linasubiri lingine liharibike, ndiyo litumike, kama halikuharibika ndiyo basi tena."

"Kama mimi nigekuwa Kadili, saa hizi ningekuwa nimeshakuoa." Maneno hayo yalimtoka Meze bila kutarajia.

"Inawezekana wewe unajua thamani yangu na si rafiki yako."

"Hakika, Eliza wewe ni mwanamke mrembo, mwenye kila sifa ya kuwa malkia ndani ya nyumba. Bahati hii haikunikuta mimi, nisingeipoteza."

"Haijakukuta kwa sasa, lakini huenda baadaye ikakukuta." Alijibu Eliza huku akiondoka taratibu kwa madaha na kumuacha Meze na maswali mengi na kitu moyoni.

"Labda maneno haya ya mwisho kuna mtu aliyasikia na kuja kumwambia shangazi." aliwaza Eliza baada ya kumaliza kurudisha akili yake nyuma, alichokuwa akizungumza na Meze jana yake usiku.

"Naona Kadili wewe umekuwa kimya tu kwa muda mrefu, mbona huchangii kitu, wakati mwenzio zimeletwa tuhuma hizi juu yake?" Mama alimuuliza Kadili.

Muda wote alikuwa ameinamia chini. Aliinua kichwa na kuwatazama wote wawili kwa zamu.

"Mama mimi nitasema kwa kifupi tu. Mimi si ndiyo mmeniteua kuwa mchumba wa Eliza?"

"Ndiyo." Mama Kadili alijibu haraka haraka. "Na Eliza si alikwenda kwa Meze kuniulizia mimi mchumba wake mtarajiwa?"

"Sawa kabisa."

"Sasa hapo ana kosa gani?"

"Hili la kuwa na uhusiano usiofaa na rafiki yako hujalisikia?" Mama aliuliza.

Kadili alitoa kicheko cha madaha, akionekana kama mtu ambaye hajali chochote kilichotokea na kushangaza mama yake.

"Mama hakuna kitu kama hicho, namfahamu Meze na namfahamu Eliza hawawezi kufanya kitu kama hiki." Alijibu kwa kujiamini kabisa kiasi cha kuwashangaza wote wawili.

"Mama huu ni uongo na usiwe na wasiwasi. Hawa wawili kama watakuwa na uhusiano wa kimapenzi, mtu wa kwanza kufahamu nitakuwa mimi na siyo wewe mama wala mtu mwingine yoyote, kwa hiyo ulicholetewa hapa ni majungu na ndiyo maana sikutaka kuongea lolote."

Mama Kadili alichoka mwili na akili. Kwa mbali alihisi kama kuna ukweli kwenye maneno ya kijana wake.

**Itaendelea Jumamosi**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA,** SHAMBA EKA 40 MOROGORO. Linafaa kufuga na kilimo, limeshavunwa misimu 3, lina nyumba vyumba 2 na Gari inafika. Bei ml.25 zenye mjadala. Wasiliana 0718965491 / 0784653304 / 0629478005.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**SILVANOS FIDELIS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0649/0048** kilichotolewa na BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA kupitia Shule ya Sekondari MKWESE mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/GOG/RB/566062/2019.**

115563202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 310..2019**

**Mdai: OMARI SHABANI DIBAGULA**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: SUMA JKT**

**Kwa: SUMA JKT WA NANENANE**

**Ombi la Mdai: OMARI SHABANI DIBAGULA**

**Madai ya: PESA ZA MKOPO WA TRECTA TSH.14,900,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 24 mwezi 12 mwaka 2019 saa 02:00 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

**Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 19 mwezi 12 mwaka 2019.**

HAKIMU YA MWANZO
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

115563302

## KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI

**MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD** anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki zenye namba za usajili **MC 150 CJX na MC 154 CJX AINA YA BOXER.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/568701/2019.**

115562902

Uza, Chenye Thamani

Kubwa Kwa

Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO




# AUBAMEYANG AJIPANGA KUONDOKA ARSENAL

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang ameripotiwa kwamba anataka kuondoka kwa miamba hao wa London Kaskazini kutokana na kuhitaji chagamoto mpya ya kutwaa mataji sehemu nyingine.

Kwa mujibu wa gazeti la Independent, mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon hana mpango wa kuongeza mkataba wa muda mrefu hapo kwenye dimba la Emirates wakati akitaka kujiunga na klabu itakayomuwezesha kushinda mataji.

Majaliwa ya Aubameyang klabuni hapo yamekuwa kwenye mashaka huku mshindi huyo wa Kiatu cha Dhahabu msimu uliopita akionyesha hana nia ya kuongeza mkataba wake, ambao utamalizika miezi 18 ijayo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ni mmoja wa wachezaji wengi ambao hawana mpango wa kuongeza mkataba na klabu hiyo, akiwamo, Alexandre Lacazette na Granit Xhaka.

Huku Mikel Arteta, jana akitarajiwa kutangazwa kuwa kocha mpya wa klabu hiyo, atakabiliwa na kazi ya ziada ya kuwashawishi wachezaji kubakia katika timu hiyo.

# Klopp: Minamino ametua Liver na kipaji cha ajabu

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp amesifia uwezo wa Takumi Minamino wakati akimkaribisha Liverpool na kubainisha kwamba wamesajili mchezaji mwenye kipaji cha "maajabu".

Kiungo huyo wa Salzburg, Minamino atajiunga na vinara hao wa Ligi Kuu ya England Januari Mosi mwakani baada ya kufuzu vipimo vya afya na kusaini mkataba wa muda mrefu Jumatatu.

Wekundu hao wameripotiwa kutoa kiasi cha pauni milioni 7.25 kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.


Klopp amesema anatarajia mengi kutoka kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Japan.

"Hizi ni taarifa njema, tumesajili mchezaji mwenye kipaji cha maajabu. Kwa uhaika tuna furaha kuhusu hilo," alisema Klopp akinukuliwa na tovuti ya Liverpool.

"Mashabiki wetu watakuwa na nafasi ya kumuona yeye kwa karibu, hivyo sihitaji kuimba kwa sauti kuhusu ubora wake, kila mmoja aliyemuona uwanjani anamjua vizuri.

"Takumi ni mchezaji mwenye kasi, akili na anajua kujipanga uwanjani. Ni shujaa akiwa na mpira ana uwezo wa aina yake. Yeye ni mchezaji anayehitajika Liverpool."

Minamino alijiunga na Salzburg akitokea Cerezo Osaka Januari 2015 na alifunga mabao 64 katika mechi 199 alizoichezea klabu hiyo ya Austria, akitoa pasi za mwisho 44.






# *Ubelgiji timu bora 2019*

**BRUSSLES,** Ubelgiji

UBELGIJI imetwaa tuzo ya timu bora ya mwaka ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), ikimaliza nafasi ya kwanza kwenye viwango vya ubora kwa Desemba ikiwa ni kwa mara ya pili mfululizo.

Kikosi hicho cha kocha, Roberto Martinez kitamaliza mwaka 2019 kikiwa kileleni kwenye viwango vya ubora baada ya kushinda mechi zake zote 10 za kimataifa mwaka huu na kufuzu kucheza Euro 2020.

Mabingwa wa Dunia, Ufaransa wanamaliza mwaka wakiwa nafasi ya pili, huku Brazil ikiwa ya tatu, England ya nne na Uruguay ya tano.

Washindi wa pili wa Kombe la Dunia, Croatia na washindi wa michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, Ureno wameungana na Hispania, Argentina na Colombia kwenye 10 bora.

HABARI MICHEZO

# Liverpool ni waathirika wa mataji, adai Lallana

**LIVERPOOL,** England

ADAM Lallana amesema Liverpool 'imeathirika' na kutwaa mataji wakati mabingwa hao watetezi wa Kombe la Ligi yaMabingwa Ulaya wakijiandaa kuongeza taji la Klabu Bingwa Dunia.

Liverpool watacheza na mabingwa wa Copa Libertadores kutoka nchini Brazil, Flamengo leo Jumamosi kwenye fainali ya Klabu Bingwa Dunia mjini Doha nchini Qatar.

Ni nafasi nyingine kwa vinara hao wa Ligi Kuu ya England, Liverpool, ambao wanapambana kushinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu tangu mwaka 1990 – chini ya kocha, Jurgen Klopp, wakiwa wameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na UEFA Super mwaka huu.

Mshambuliaji wa Liverpool Lallana alisema: "Ni kubwa. Sisi ni Mabingwa wa Ulaya na tunataka kutwaa taji la Klabu Bingwa ya Dunia sio wengi wanaoweza kusema hivyo.

"Tutakwenda kupambana. Ni kama tumeathirika: unashinda taji na unataka kushinda tena. Unataka kushinda zaidi."

Liverpool ilitinga fainali hiyo baada ya kuifunga Monterrey 2-1 shukrani kwa bao la Roberto Firmino la dakika za majeruhi.

Flamengo, ambao waliwafunga River Plate kwenye fainali ya Libertadores, waliwatoa Al Hilal wakimaliza na wachezaji 10 uwanjani wakati wakishinda 3-1 kwenye nusu fainali.

"Utakuwa mchezo mgumu," alisema Lallana. "Nina uhakika Bobby (Firmino) na Alisson watatupa kitu kizuri."



# DESCHAMPS AMPA NAFASI ZIDANE KUINOA UFARANSA



**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps anaamini kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane atawanoa mabingwa hao wa Kombe la Dunia 2018, hivi karibuni au baadaye.

Zidane yupo katika kipindi chake ha pili kuinoa Madrid, akiwa amerudi Machi mwaka huu baada ya kujiuzulu Mei mwaka 2018 kufuatia kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo pamoja na lile la LaLiga.

Mfaransa huyo na nahodha wa zamani wa Les Bleus hao, ambaye alishinda Kombe la Dunia mwaka 1998, kwa muda mrefu amekuwa akichukuliwa kama mrithi wa Deschamps.

Wakati Deschamps ataendelea kuwa kocha wa Ufaransa hadi kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2022, kocha huyo mwenye umri wa miaka 51, anamuona Zidane ndiye anafaa kuwa mrithi wake.

"Kocha ajaye anaweza kuwa Zizou," alisema Deschamps, ambaye amekuwa kocha tangu mwaka 2012, amesema Le Monde.

"Kwa upande mmoja au mwingine, anaweza kuwa yeye."

Deschamps aliongeza mkataba wake kuiongoza timu hiyo hadi mwaka 2022 baada ya kuifunga Croatia kwenye fainali ya mwaka jana.

# *Pochettino atarudi Spurs-Levy*

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino siku moja anaweza kurudi kwa mara ya pili kuinoa Tottenham, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Daniel Levy amebainisha.

Pochettino - ambaye aliiongoza Spurs kumaliza kwenye nne bora katika misimu minne mfululizo kwenye Ligi Kuu, pamoja na fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya - alifukuzwa Novemba mwaka huu kwa matokeo mabaya.

Jose Mourinho aliteuliwa kuwa mrithi wake, huku Spurs ikishinda mechi tano kati ya saba kwenye mashindano yote hadi sasa.

Levy amedokeza kwamba kufukuzwa kwa Pochettino hakumaanishi kwamba kunaweza kuwa mwisho kwa raia huyo wa Argentina kujihusisha na Spurs.

"Mnatakiwa kuelewa, nilijenga uhusiano mzuri na Mauricio kwa kipindi cha miaka mitano na nusu," alisema Levy akiliambia gazeti la Evening Standard.

"Si kitu nilichokipenda. Binafsi ilikuwa ni ngumu, nilimwabia na akaelewa.

"Amekuwa kwenye soka kwa muda mrefu, anaelewa. Si mambo binafsi na nina uhakika atarudi akiwa na nguvu mpya na atakuwa na nafasi ya kuinoa klabu. Pengine siku moja atarudi kwetu.

"Niwezi kukaa hapa na kuelezea yaliyopita. Mauricio alifanya kazi ya kuvutia na sisi, namtakia kila la heri.

"Bado nina mawasiliano naye. Mahusiano yetu ni mazuri tu na tutaendelea kuwasiliana kila inapobidi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH ANA VIVULI VYA MESSI, ADAI WENGER

●●● Anafunga na kutoa pasi za mwisho, huyo ni mchezaji aliyekamilika, wote tunatamani...

**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah anacheza kwa kiwango sawa na ubora wa Lionel Messi, kwa mujibu wa kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger.

Salah, ambaye alishinda tuzo ya Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu England kwa misimu miwili iliyopita - ingawa msimu wa 2018-19 aliitwaa kwa pamoja na mchezaji mwenza wa Liverpool, Sadio Mane na straika wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, tayari mshambuliaji huyo raia wa Misri ana mabao 13 kwa jina lake katika mashindano yote msimu huu.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Roma pia ameshatoa pasi za mwisho saba msimu huu ikiwa ni pamoja na aliyompasia Naby Keita wakati akifunga bao la kwanza Liverpool ikishinda 2-1 dhidi ya Monterrey kwenye mechi ya nusu fainali ya Klabu Bingwa Dunia, Jumatano.

**Na wakati Mmisri huyo akipiga hatua kwa kubeba jukumu la kiungo mchezeshaji pamoja na mmaliziaji, Wenger anaamini Salah sasa anaonyesha mwangaza wa kucheza kwa kiwango sawa na nyota wa Barcelona na mshindi wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] 2019, Messi.**

"Napenda mageuzi yake," Wenger aliiambia beIN Sports. "Kwa sababu alikuwa na ugusaji [dhidi ya Monterrey] wa kiungo mchezeshaji.

"Alitengeneza nafasi kuzunguka boksi ambao ni wa kipekee, kulikuwa na vivuli vya Messi ndani yake na ninapenda mtu ambaye anaweza kufunga lakini pia akiweza kutoa pasi za mwisho.

"Huyo ni mchezaji aliyekamilika. Ndiyo maana wote tunatamani na ndicho tunachokihitaji kutoka kwa wachezaji."

Wenger alikuwa akiongea kwenye mahojiano ya pamoja na Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, ambaye alielezea kauli ya Mfaransa huyo.

"Vizuri sana, vizuri sana uzoefu [na Salah] lakini yaliyo chanya zaidi ni katika uwanja wa mazoezi - nzuri kihisia," Klopp alisema. "Uwanjani ni mkubwa, kweli, nzuri sana."

Liverpool itawavaa mabingwa wa Copa Libertadores, Flamengo kwenye mechi ya fainali ya Klabu Bingwa Dunia leo, Jumamosi.

## ZISIKUPITE

### OZIL KUTUA FENERBAHCE

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil, 31, anajiandaa kujiunga na Fenerbahce ya Uturuki kwa mkataba wa mkopo wa miezi sita katika dirisha la usajili la Januari. ***(Fotomac, via Football.London)***

### POGBA KUZUIWA JANUARI

MANCHESTER United haitamruhusu kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, kuondoka Real Madrid Januari. ***(Mail)***

### KUANZA NA IBRAHIMOVIC

KAMA Carlo Ancelotti atatangazwa kuwa kocha wa Everton usajili wake wa kwanza utakuwa ni kujaribu kuinasa saini ya mshambuliaji wa zamani wa Manchester United, Zlatan Ibrahimovic, 38. Msweden huyo atakuwa mchezaji huru kuanzia Januari Mosi, mwakani wakati mkataba wake na LA Galaxy utakapomalizika. ***(Calcio Mercato)***

### CHELSEA NAYO KWA VINICIUS

CHELSEA ni miongoni mwa klabu za Ligi Kuu England zinazofukuzia saini ya winga wa Real Madrid na Brazil, Vinicius Junior, 19, katika dirisha la Januari. ***(El Desmarque, via Star)***

### CAN KUOMBA KUONDOA JUVE

KIUNGO wa zamani wa Liverpool na Ujerumani, Emre Can, 25, anaweza kuwasilisha ombi la kuondoka Juventus kufuatia kuendelea kupata wakati mgumu wa kuanza kikosi cha kwanza. ***(Goal)***

### UNITED, CITY KWA HAVERTZ

ZOTE Manchester City na Manchester United zimefanya "mazungumzo ya kina" ya kumsajili kiungo wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Kai Havertz, 20. ***(Manchester Evening News)***

### AUBAMEYANG ANUKIA KUSEPA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 30, anaongoza idadi kubwa ya wachezaji wa 'Gunners' wanaofikiria mustakabali wao wa baadaye klabuni hapo. ***(Independent)***

### BORINI AWINDWA PALACE

CRYSTAL Palace inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Liverpool na Sunderland, Fabio Borini, wakati huu Muitaliano huyo kwa sasa akiwa AC Milan. ***(Corriere Dello Sport, via Sport Witness)***

### HAALAND KUMTOA RAIOLA

MANCHESTER United inaweza kulazimika kulipa pauni milioni 12 kama ada kwa wakala Mino Raiola ili kupanda dau la ada ya uhamisho wa ya mshambuliaji wa RB Salzburg na Norway, Erling Braut Haaland, 19. ***(Sun)***

### MOURA AITAJA UTD KWA PSG

KIUNGO wa Tottenham na Brazil, Lucas Moura, 27, amekiri kuwa alikaribia kujiunga na Manchester United mwaka 2012 kabla ya mwishoni kuamua kutua Paris St-Germain badala yake. ***(ESPN Brasil, via Mirror)***

### KING KURUDISHWA LEICESTER

RANGERS inajiandaa kuhitimisha mapema mkataba wa mkopo wa muda mrefu na kiungo Andy King, 31, na kumuacha nyota huyo wa kimataifa wa Wales kurudi Leicester. ***(Daily Record)***

HABARI MICHEZO

# U-20 waitia kiburi usajili Mtibwa Sugar

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU dirisha dogo la usajili Tanzania Bara likipamba moto kwa klabu za Ligi Kuu kuanza kujiimarisha kwa kusajili kwa kasi, mabingwa mara mbili wa ligi hiyo, Mtibwa Sugar wamesema hawatafanya 'fujo' yoyote sokoni na badala yake watamulika katika kikosi chao cha vijana wa umri chini ya miaka 20.

Dirisha dogo la usajili limefunguliwa tangu Desemba 16, mwaka huu na linatarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani na tayari klabu zipo sokoni kuimarisha vikosi vyao.

Akizungumza na mwandishi wetu, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobius Kifaru, alisema hawana sababu ya kuongeza wachezaji wapya kutoka nje wakati wana vijana wazuri wenye uwezo wa kuisaidia timu hiyo iliyopo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 19 baada ya kushuka dimbani mara 13.

"Tumeshatwaa ubingwa wa Ligi Kuu mara mbili tukiwa na vijana, hatuna sababu ya kusajili kutoka nje wakati tumewekeza sana kwa vijana, kama kocha atahitaji kuimarisha kikosi chake atapandisha vijana kutoka kikosi cha U-20.

"Tunaamini watatoa changamoto kubwa kwani wapo vizuri kwa asilimia zaidi ya 90, kazi yetu huwa ni kuzalisha vijana na hilo kila mtu analijua," alisema Kifaru.

Mtibwa Sugar ni miongoni mwa timu zinazoaminika kwa kuzalisha vijana na imekuwa ikipandisha wachezaji wengi kutoka kikosi chake cha U-20 ambao wengi hushia kusajiliwa na klabu kubwa hususan Simba na Yanga baada ya kung'ara wakiwa na timu ya wakubwa ya 'Wakata Miwa' hao wa Manungu mkoani Morogoro.

# SIMBA MO ARENA WAIKUNA TFF SIMBA QUEENS IKIICHAPA MARSH

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba Queens, ikizindua Uwanja wa Simba Mo Arena kwa ushindi wa mabao 3-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu uliopigwa dimbani hapo jana, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limekunwa na ubora na viwango vya viwanja hivyo vya Wekundu wa Msimbazi vilivyopo Bunju, jijini Dar es Salaam.

Simba Queens jana iliikaribisha Marsh Queens kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake, ambao huo ulikuwa mchezo wa kwanza wa kimashindano kupigwa Uwanja wa Simba Mo Arena tangu ulipozinduliwa, ambao ulishuhudiwa na mashabiki wengi.

Sambamba na mechi hiyo, Mkurugenzi wa Ufundi wa TFF, Oscar Mirambo, alipata fursa ya kutembelea Simba Mo Arena jana na kueleza kufurahishwa na hatua klabu hiyo iliyofikia kwa kumiliki viwanja vyake viwili vya mazoezi, kimoja cha nyasi bandia na kingine nyasi asili.

**"Niwapongeze Simba kwa hatua ambayo wamepiga kwa kuwa na viwanja ambavyo tumekuwa na uhaba navyo. Hii inamaana kwamba kama nchi sasa tunapiga hatua," alisema Mirambo baada ya kutembelea Simba Mo Arena.**

Kikosi cha Wanaume cha Simba, kimekuwa kikifanya mazoezi katika viwanja hivyo tangu vilipozinduliwa kwa kukabidhiwa kwa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo Desemba 7, mwaka huu.

Hata hivyo, hatua hiyo inaelezwa ni ya awali na klabu hiyo ipo katika mchakato wa kushirikisha mashabiki kuchangia hela kwa ajili ujenzi wa uzio wa ukuta pamoja na hosteli za wachezaji, ujenzi ambao unatarajiwa kwenda sambamba na akademi ya soka.

Tayari mwekezaji bilionea wa klabu hiyo , Mohamed 'Mo' Dewji ameahidi kutoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuchangia ujenzi huo unaoelezwa utagharimu jumla ya Sh. bilioni mbili.

USIYEMPENDA KAJA...



Beki Andrew Vincent Chikupe 'Dante' (kulia), akipeana mkono na Katibu Mkuu, David Luhago, baada ya kumaliza tofauti zake za klabu na kurejea rasmi kazini kutokana na mgomo wake tangu Agosti akishinikiza alipwe malimbikizo ya fedha zake za usajili. Dante ni miongoni mwa mabeki nchini ambao washambuliaji hawapendi kukutana naye kutokana na kuwapa tabu uwanjani. **PICHA: YANGA**

KARUDI...



Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Mhandsi Hersi Said (kushoto), akimtambulisha Haruna Niyonzima baada ya kusaini mkataba wa kujiunga tena na timu hiyo mjini Kigali jana. **PICHA: YANGA**

# *Niyonzima awatuliza mashabiki Yanga*

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Yanga kwa mara nyingine tena imemsajili kiungo fundi aliyeichezea timu hiyo kabla ya kujiunga na Simba na baadaye kurejea kuitumikia klabu ya kwao Rwanda, AS Kigali.

Niyonzima alitambulishwa na Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Mhandsi Hersi Said, baada ya Mnyarwanda huyo kusaini mkataba wa kuitumikia klabu hiyo jana mjini Kigali, Rwanda.

Huku baadhi ya mashabiki wakibeza uwezo wa kiungo huyu mnyumbulifu, Niyonzima ambaye kwa sasa ni nahodha wa AS Kigali, amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kwa kuwaeleza anakuja kupambana.

Niyonzima ni miongoni mwa wachezaji wapya ambao wamekamilisha kutia saini ya kujiunga na Yanga katika dirisha hili dogo, wengine wakiwa ni mshambuliaji Tariq Seif aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Misri, beki wa kushoto kutoka JKT Tanzania, Adeyun Saleh Ahmad pamoja na straika Ditram Nchimbi aliyekuwa akiichezea Polisi Tanzania kwa mkopo akitokea Azam FC.

"Nafahamu nilipoondoka mashabiki wa Yanga hawakupenda, lakini maslahi ndiyo yaliyoniondoa siyo kingine, nilikwenda huko sikuwa na upepo nao mzuri na ndiyo maana mkataba wangu ulivyoisha niliamua kuondoka.

"Ninarejea tena Yanga ikiwa ni klabu iliyonilea, kunikuza na kunifikisha hapa nilipo, hivyo ninakuja kwenye timu ninayoipenda, naahidi kuipambania kwa kipindi chote nitakachokuwapo hapo," alisema Niyonzima maarufu kama Fabregas. Yanga inatajiwa kushuka Uwanja wa Uhuru leo kuikaribisha Iringa United kwenye mechi ya kuwania Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF) maarufu kama FA Cup.

Bingwa wa michuano hiyo, hupata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Michezo

Jumamosi Desemba 21, 2019

Nipashe




Salah ana vivuli vya Messi, adai Wenger HABARI UK.30

## SIMBA MO ARENA KWANOGA...



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi katika Uwanja wao wa Simba Mo Arena, Bunju jijini Dar es Salaam jana, kujiandaa na mechi za Ligi Kuu sambamba na mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Arusha United. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Aussems atajwa Yanga

## ●●● Kikosi chazidi kunoga, Niyonzima, Nchimbi rasmi, Dante naye arejea huku straika Muivory Coast akitua...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ikidizi kujiimarisha katika usajili wa dirisha dogo kwa kusajili wachezaji nyota wa kuziba mapengo yaliyojitokeza, aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, ametajwa kuwa ni miongoni mwa makocha walioomba kazi ya kuwanoa mabingwa hao wa kihistoria nchini, Klabu ya Yanga, imeelezwa.

**Tangu kufunguliwa kwa dirisha dogo Desema 16, mwaka huu, Yanga inayonolewa na Kaimu Kocha Mkuu, Boniface Mkwasa baada ya Kocha Mkuu Mwinyi Zahera kutimuliwa, imekuwa 'bize' na usajili huku suala la kutafuta kocha mkuu likionekana kupoa kwa sasa.**

Hata hivyo, juzi usiku ziliibuka taarifa kuwa Aussems ni miongoni mwa makocha walioomba kuinoa timu hiyo iliyopo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na alama 17 baada ya kushuka dimbani mara nane msimu huu.

Lakini alipoulizwa Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, hakuwa tayari kulizungumzia suala hilo zaidi ya kusema kwa sasa wanashughulikia kwanza usajili na hana taarifa hizo za Aussems kuomba kazi katika klabu hiyo.

"Sina taarifa hizo, kama kuna kitu kama hicho hakijafika mezani kwangu, naomba muwe na subra kwanza kwa sasa," alisema.

Kwa upande wa usajili, klabu hiyo imefanikiwa rasmi kuinasa saini ya kiungo mnyumbulifu, Mnyarwanda Haruna Niyonzima anayeitumikia AS Kigali ya kwao, Rwanda sambamba na straika Ditram Nchimbi aliyekuwa akiichezea Polisi Tanzania kwa mkopo akitokea Azam FC.

Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Mhandsi Hersi Said, ndiye aliyemtambulisha Niyonzima baada ya kusaini mkataba wa kujiunga tena na timu hiyo mjini Kigali jana hiyo ikiwa ni baada ya juzi kumtambulisha Nchimbi kufuatia kutia saini mkataba wa miaka miwili wa kujiunga na miamba hiyo akiwa jijini Kampala, Uganda kwenye michuano ya Kombe la Chalenji iliyomalizika Alhamisi wiki hii.

"Welcome back fundi Haruna Niyonzima. Shukran sana kwa @gsmtanzania kwa kulisimamia hili," ilisomeka taarifa ya Yanga jana huku pia ikifuatiwa na nyingine iliyosomeka. "Karibu Jangwani Ditram Nchimbi. Shukran sana kwa @gsmtanzania kwa kulisimamia hili."

Wakati usajili ukikamilika kwa wachezaji hao ambao sasa wanaungana na Tariq Seif, na beki wa kushoto Adeyun Saleh Ahmad waliosajiliwa katika dirisha hili, Mkurugenzi wa Mashindano wa klabu hiyo, Thabit Kandoro jana alimpokea mshambuliaji Muivory Coast, Gislein Yikpe Gnamian aliyekuwa anachezea Gor Mahia ya Kenya baada ya kuwasili kwa ajili ya kujiunga na Yanga.

## Aubameyang sasa kuondoka Arsenal

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang...



HABARI UK 28

## Pochettino atarudi Tottenham – Levy

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino siku moja anaweza kurudi kwa mara ya...



HABARI UK 29

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >